# IKULU ZANZIBAR

SERIKALI KWA MAENDELEO YA WANANCHI

TOLEO NO. 019 ISSN 1821 - 8253 JANUARI - FEBRUARI 2015



## Rais wa Ujerumani ausifu Utamaduni, Mila na Silka za watu wa Zanzibar

## Bodi ya Wahariri

**Mhariri Mkuu**
Hassan K. Hassan

**Mhariri Msaidizi**
Ali S. Hafidh

**Waandishi**
Said J.Ameir
Rajab Y. Mkasaba
Haji M. Ussi
Said K. Salim
Yunus S. Hassan
Mahfoudha M. Ali
Amina M. Ameir

**Mpiga Picha**
Ramadhan O. Abdalla

**Msanifu**
Aziz I. Suwed


## UTAMBULISHO

Wapenzi wasomaji wa Jarida la Ikulu tunafuraha kukukaribisheni katika uendelezaji wa juhudi za Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuimarisha mawasiliano na wananchi.

Ni lengo la Ofisi ya Rais kukuza mawasiliano na wananchi kwa kutumia njia tofauti kama vile Jarida, vipeperushi pamoja na vyombo vyengine vya habari.

Tunakaribisha maoni yenu ili tuweze kufikia lengo hilo.


Jarida hili limetolewa na Idara ya Mawasiliano Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar.



P.O.BOX: 2422

Zanzibar - Tanzania

Phone: +255 223 081/5

Fax: 024 223 3722

Email: com_ikulu@ikuluzanzibar.go.tz


# Maoni ya Mhariri

## Tulidhamiria na tumeweza

Mwishoni mwa mwezi Februari, 2015, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein, amekamilisha duru nyengine ya vikao vya Wizara zote 16 za Serikali, ambavyo hukutana kujadili utekelezaji wa bajeti na mpango kazi kwa kila Wizara kwa kipindi maalum, kama itakavyoelekezwa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Vikao vya mwisho vilivyoishia mwishoni mwa mwezi wa Februari 2015, vilijadili utekelezaji wa bajeti na mpangokazi kwa kila Wizara kwa kipindi cha Julai – Disemba 2015.

Utaratibu wa kufanya vikao hivyo ni wa kwanza wa aina yake, kwa maana kwamba havikuwahi kufanywa na kiongozi yeyote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tokea kuasisiwa kwa Serikali hiyo ambayo imedumu kwa zaidi ya miaka 51 sasa.

Ni ukweli uliowazi kwamba, kuanzishwa kwa utaratibu huo mpya kulijenga hofu miongoni mwa baadhi ya watendaji, siyo tu kwa kudhani kwamba watendaji watatakiwa kujibu hoja nzito zitakazojitokeza wakati wakitekeleza majukumu yao, lakini vile vile haikuwa jambo la kawaida kwa baadhi ya watendaji na hasa katika ngazi ya wakurugenzi, kukutana ana kwa ana na Mheshimiwa Rais, Makamo wa Kwanza wa Rais, Makamo wa Pili wa Rais, na kujadiliana nao masuala ya kazi zao mbele ya wakuu wao wa kazi kama vile Makatibu wakuu na Mawaziri.

Kama ilivyo kwenye vikao vingine rasmi vyenye kujadili masuala muhimu ya maendeleo ya nchi, vikao vya kujadili utekelezaji wa mpango kazi na bajeti kwa Wizara zote za Serikali chini ya uenyekiti wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, hufanyika bila ya kuingizwa itikadi za kisiasa na ni vigumu kubaini itikadi za washiriki wakati vikao hivyo vinapokuwa vikiendelea, jambo ambalo kwa mara nyengine tena linathibitisha kuwa tukidhamiria wenyewe tunaweza.

Miongoni mwa masuala muhimu yanayojadiliwa kwenye vikao hivyo ambavyo vinajulikana kwa jina la bango kitita, ni kuangalia utekelezaji wa maagizo mbali mbali yanayotolewa kwenye vikao vilivyotangulia, uingizwaji wa fedha kwa kila Idara na namna fedha hizo zilivyotumika. Aidha, vikao vinaangalia thamani ya fedha na matumizi halisi yaliyofanywa kwa fedha hizo.

Faraja kubwa wanayoipata washiriki wa vikao hivyo ni kupata fursa ya kutoa maoni yao kuhusiana na jambo lolote linalowakwaza katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku kwenye sehemu zao za kazi, na vile vile kuishauri Serikali namna bora zaidi ambayo kwa maoni yao itaongeza ufanisi na hatimaye kuimarisha huduma bora kwa jamii.

Hatua hii ya ushirikishwaji wa watendaji katika kupanga na kutekeleza sera za Serikali na mipango ya maendeleo ya kitaifa inabeba uzito wa kipekee katika mfumo wa uongozi uliojikiti katika masuala ya utawala bora.

Pamoja na ukweli kwamba Serikali inazo njia nyingi za kupata taarifa za aina mbali mbali, kupitia vikao hivi vya bango kitita, Serikali inapata fursa ya kufahamu kwa undani vyanzo vya matatizo mengi ya kijamii na kuchukua hatua za haraka kuyapatia ufumbuzi kabla ya matatizo hayo kugeuka kuwa kero ndani ya jamii.

Uzoefu wa miaka minne ya vikao hivyo umeonesha kuwa vikao vya kutathmini utekelezaji wa mpango kazi na bajeti katika vipindi tofauti siyo tu vimekuwa vikichochea kasi ya utekelezaji wa majukumu ya taasisi za Serikali, lakini vile vile vimekuwa chimbuko la mambo muhimu yenye kuleta maslahi makubwa katika jamii.

Vile vile vikao hivyo vimekuwa vikiongeza kasi ya uwajibikaji kwa watendaji wote wa Serikali, ambao wanatekeleza majukumu yao kwa tahadhari kubwa, huku wakijua kwamba watahojiwa kuhusiana na mafanikio na changamoto wanazokabiliana nazo katika kutekeleza shughuli walizoziombea fedha za umma.

Mpango huu wa mikutano ya bango kitita unaitofautisha kiutendaji awamu hii ya saba ya uongozi na awamu nyengine zilizotangulia, ambazo kimsingi hoja kuhusu utekelezaji wa bajeti zilikuwa zikiibuliwa kwenye Baraza la Wawakilishi, baada ya chombo hicho kuanzishwa rasmi kikatiba mwaka 1980.

# Rais wa Ujerumani ausifu Utamaduni, Mila na Silka za watu wa Zanzibar



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na mgeni wake Rais wa Shirikisho la Serikali ya Ujerumani Mhe. Joachim Gauck katika ukumbi wa Ikulu Mjini Zanzibar alipofika na ujumbe wake tarehe 4 Februari 2015*

Zanzibar inaendelea kujijengea sifa kutokana na mila, silka na utamaduni wake wa kuheshimiana bila ya kujali tofauti za dini, rangi, kabila na itikadi za kisiasa.

Hisia na kauli ya kuvutiwa hali hiyo ilionekana wazi wazi kwenye uso na kauli ya Rais wa Ujerumani Mheshimiwa Joachim Gauk wakati wa ziara yake ya kutwa moja Zanzibar ambapo, pamoja na mambo mengine alikuwa na mazungumzo na mwenyeji wake Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein.

Mheshimiwa Joachim aliwasili majira ya asubuhi kwa boti inayomilikiwa na Kampuni ya Azam Marine akitokea mjini Dar es Salaam na alilakiwa na mwenyeji wake Dk. Ali Mohamed Shein kwenye Bandari ya Malindi, Zanzibar.

Mara baada ya kuwasili, kama ilivyo kawaida kwa wageni wakuu wa kiserikali, Mheshimiwa Rais wa Shirikisho la Serikali ya Ujerumani alikagua gwaride rasmi la Jeshi la Wananchi wa Tanzania na kupigiwa mizinga 21.

Tumbuizo za ngoma za asili za kibati na ndege zilikuwa ni hatua ya kwanza ya mamia ya wananchi wa Zanzibar waliokuwa wamejipanga barabarani kumlaki kiongozi huyo ambaye aliamua kutembea kwa miguu kutoka Bandari ya Malindi Zanzibar hadi kwenye hoteli ya Serena.

Masafa hayo ya kiasi cha mita 250 yalimpa fursa nzuri kiongozi huyo kutoka moja kati ya mataifa makubwa duniani kujionea kwa macho yake mji Mkongwe wa Zanzibar wenye hadhi ya kimataifa, na angalau kwa kiasi kidogo kusoma na kufahamu mila, silka na utamaduni wa wananchi wa Zanzibar.

Ratiba ya ziara ya Rais wa Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani ilimchukua hadi Ikulu Zanzibar ambako alikutana na kufanya mazungumzo na mwenyeji wake Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na mgeni wake Rais wa Shirikisho la Serikali ya Ujerumani Mhe. Joachim Gauck mara alipowasili katika Bandari ya Malindi Mjini Zanzibar akitokea Dar es Salaam tarehe 4 Februari, 2015*

wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein ambaye alimuelezea mgeni wake hali halisi ya Zanzibar kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni.

Kimsingi ziara ya Rais wa Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani, Mheshimiwa Joachim Gauck nchini, ni fursa nyingine muhimu ya kuimarisha uhusiano na ushirikiano uliopo kati ya Zanzibar na Ujerumani. Katika mazungumzo yake na kiongozi huyo, Dk. Shein amesema kuwa historia inaonesha kuwa uhusiano kati ya Zanzibar na Ujerumani ulianza mwaka 1847 ikiwa ni nchi ya tatu baada ya Marekani na Uingereza kuanzisha mahusiano na Zanzibar.

"tumefurahi ziara yako itaimarisha urafiki na uhusiano wetu kwa kuendelea kushirikiana katika maeneo ambayo tayari tunashirikiana sasa na hata kuanzisha maeneo mengine mapya", Dk. Shein alimueleza Rais Gauck.

Miongoni mwa mambo muhimu ambayo Rais wa Ujerumani alivutiwa navyo, ni namna ambavyo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye muundo wa Umoja wa Kitaifa inavyoendesha shughuli zake kwa mafanikio makubwa ikijumuisha viongozi wa vyama ambavyo kwa muda mrefu vilikuwa vikihasimiana.

Aidha, kiongozi huyo wa Ujerumani alionekana mwenye hamu kubwa ya kujua namna Zanzibar inavyoendelea kudumu na amani na utulivu huku kukiwa na watu waliochanganyika kiitikadi wakiwemo wafuasi wa makundi ya dini tofauti.

Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jumla, zinajivunia uhusiano na ushirikiano mzuri wa kidiplomasia, kiuchumi na kibiashara uliopo kati yake na Ujerumani. Ni dhahiri, ziara hii ya Rais wa Ujerumani siyo tu inatoa fursa nyengine ya kupanua ushirikano ambao umedumu kwa muda mrefu sasa, lakini vile vile inafungua ukurasa mwengine wa kuanzisha maeneo mapya ya ushirikiano baina ya pande hizo mbili.

Itakumbukwa kuwa, zaidi ya msaada wa kibajeti kupitia "General Budget Support – GBS", Ujerumani imekuwa mshirika mkuu wa maendeleo Zanzibar ikiisaidia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika maeneo mbali mbali kwa lengo la kuinua ukuaji wa uchumi na hali za maisha ya jamii kwa jumla.

Maeneo mengine ambayo yanaweza kutumika kupanua wigo wa ushirikiano ni pamoja na Zanzibar kutumia fursa hiyo kushirikiana na Ujerumani kwa kuanzisha ushirikiano baina ya taasisi ya Utafiti ya Kizimbani na taasisi za aina hiyo nchini Ujerumani kwa kubadilishana programu baina ya taasisi hizo hasa katika masuala ya kilimo cha kisasa ambayo Ujerumani imepiga hatua kubwa.

Miongoni mwa maeneo ambayo ujumbe wa Wawekezaji wa Ujerumani uliofuatana na Rais Joachim Gauck umekuwa na hamu ya kuyaendeleza, ni pamoja na kuwekeza katika sekta ya mafuta na gesi, kilimo na usalama wa chakula, mifugo, uvuvi, mawasiliano, maendeleo ya miundombinu na utalii ambapo Serikali zote mbili nazo zimekuwa na mkakati maalum wa kuyaendeleza.

Rais wa Zanzibar pamoja na mambo mengine aliitumia fursa hiyo kuishukuru Serikali ya Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani kwa misaada yake mbali mbali inayoitoa kuunga mkono jitihada za wananchi za kujiletea maendeleo.

"Tunaishukuru serikali na wananchi wa Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani kwa kuendelea kuisaidia Tanzania katika jitihada zetu za kujiletea maendeleo na kufanya hivyo sisi tunawaona nyinyi kuwa ni wenzetu na marafiki wa kweli" Dk. Shein alisema.

Alitaja baadhi ya maeneo ambayo Ujerumani inaisaidia Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kuwa ni pamoja na hifadhi ya mazingira, msaada katika bajeti, nishati na huduma za jamii.

Kwa hivyo Dk. Shein alimueleza Rais wa Ujerumani kuwa Zanzibar na Tanzania kwa jumla zingependa kuona nchi hizo zinashirikiana katika maeneo mapya ya kiuchumi na biashara ikiwemo uwekezaji katika sekta ya utalii.

Katika mazungumzo yao, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein vile vile alimueleza Rais wa Ujerumani kuwa mafanikio yaliyopatikana hivi sasa Zanzibar yanatokana na wananchi kuishi kwa amani na utulivu huku wakizingatia uvumilivu wa kisiasa na kidini.

"Tumekuwa na ustahamilivu wa kidini Zanzibar kwa karne nyingi na katika historia ya nchi yetu, waumini wa dini zote wamekuwa wakiishi kwa mapenzi makubwa na huku

Katiba zetu zote mbili zikimpa kila mwananchi uhuru wa kuabudu dini anayoitaka" Dk. Shein alieleza.

Aliongeza kuwa katika mwaka 1953 Zanzibar ilitoa stempu maalum ya kuonesha ustahamilivu wa kidini ambapo baadae Dk. Shein alimkabidhi mgeni wake nakala ya stampu hiyo.

Dk. Shein alimhakikishia Rais wa Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani kuwa hivi sasa Zanzibar iko katika utulivu mkubwa na kusifia ushirikiano mzuri uliopo katika Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iliyo katika mfumo wa Umoja wa Kitaifa.

"Katika miaka minne hii Serikali yetu iliyo chini ya Muundo wa Umoja wa Kitaifa imekuwa ikifanya vizuri. Tuna ushirikiano ndani ya serikali na si rahisi kufahamu tofauti zetu za kisiasa kwa kuwa lengo letu ni moja la kujenga nchi yetu" alieleza Dk. Shein.



*Rais wa Shirikisho la Serikali ya Ujerumani Mhe. Joachim Gauck akisalimiana na Wakuu wa vikosi vya ulinzi na usalama Zanzibar waliojitokeza kumpokea wakati alipowasili Bandari ya Malindi Zanzibar tarehe 4 Februari, 2015*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na mgeni wake Rais wa Shirikisho la Serikali ya Ujerumani Mhe. Joachim Gauck wakiangalia Ngoma ya Mwanandege ambayo huchezwa katika sherehe mbali mbali za Kitaifa hapa Zanzibar*



*Rais wa Shirikisho la Serikali ya Ujerumani Mhe. Joachim Gauck akisalimiana na mmoja kati ya mamia ya wakaazi wa Mji Mkongwe wa Zanzibar waliojitokeza kumlaki wakati alipokuwa akitembea kwa miguu kutoka Bandari ya Malindi Zanzibar kuelekea hoteli ya Serena tarehe 4 Februari, 2015*

Kwa upande wake Rais wa Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani Mheshimiwa Joachim Gauck alimueleza Dk. Shein kuwa amefurahi kuona Zanzibar ni nchi yenye kukusanya watu wa tamaduni nyingi pamoja na dini tofauti lakini wanaishi kwa amani na mashirikiano makubwa.

Rais huyo alieleza kuwa wananchi wa Ujerumani wanafahamu uhusiano wa kihistoria uliopo kati ya nchi yao na Zanzibar na kwamba amekuja hapa kuangalia namna nchi hiyo inavyoweza kuimarisha zaidi uhusiano huo.

Mheshimiwa Gauck alisema watu wa Ujerumani wanapata taswira nzuri ya Zanzibar kutokana na watalii wanaotembelea Zanzibar na Tanzania mara kwa mara.

Kuhusu hali ya kisiasa nchini Rais Joachim Gauck alisema "Nimefurahi kuona wananchi wa Tanzania ni watu wanaowasiliana na kujadiliana mambo yao, si watu wanaogombana na hilo ni jambo kubwa kwa maendeleo ya demokrasia".

Alisisitiza kuwa nchi yake itaendelea kushirikiana na Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jumla ili kuuenzi na kuimarisha uhusiano na ushirikiano huo wa miaka mingi.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein (katikati), Makamo wa Pili wa Rais Balozi Seif Ali Iddi (kulia), Jaji Mkuu wa Zanzibar Mheshimiwa Omar Othman Makungu, Jaji Mkuu wa Tanzania Mheshimiwa Mohamed Othman Chande (kushoto) na Waziri wa Katiba na Sheria Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakari wakiwa wamesimama wakati Wimbo wa Taifa ukipigwa katika maadhimisho ya kilele cha Siku ya Sheria zilizofanyika katika viwanja vya bustani ya Victoria Mjini Unguja tarehe 10 Februari 2015*

# Jitihada za SMZ katika kuimarisha uhuru wa Mahkama

Mfumo wa Kidemokrasia wa vyama vingi vya siasa wenye kuheshimu Utawala wa sheria, haki za binaadamu, usawa, amani, haki na uadilifu ilivyoelezwa kwenye katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, ni miongoni mwa mambo ya msingi ambayo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yenye Muundo wa Umoja wa Kitaifa imeyapa kipaumbele tokea ilipoingia madarakani zaidi ya miaka minne iliyopita.

Katika suala zima la mgawanyo wa madaraka, imeelezwa katika katiba ya Zanzibar ibara ya 5A (1) kama ifuatavyo:-

"Zanzibar itakuwa na mfumo wa mgawanyo wa madaraka kati ya Mamlaka tatu. Mamalaka ya Utendaji, Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji wa Shughuli za Umma na Mamlaka ya Kutekeleza Utoaji Haki.

(2) "Mamlaka ya Utendaji ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mamlaka ya Kutunga Sheria na Kusimamia Utekelezaji wa Shughuli za Umma ni Baraza la Wawakilishi na Mamalaka ya Kutekeleza Utoaji Haki ni Mahkama.

(3) "Hakuna Mamlaka itakayoingilia Mamlaka nyengine isipokuwa kama na kwa kadri iliyovyoelezwa katika Katiba hii".

Hivyo kwa mujibu wa katiba, mahkama ni miongoni mwa mihimili mitatu mikuu nayo inatakiwa kuwa ni chombo au taasisi huru. Uhuru kwa maana ya kuwa, wale wote waliopewa jukumu la kutoa haki ya kuamua mtu kuwa mkosa au hana hatia kikatiba, lazima awe huru kutokana na aina zote za shindikizo, bila ya kujali zinakotoka.

Vile vile Serikali siku zote inahakikisha kuwa Mahkama zinakuwa huru kutokana na shindikizo za kisiasa, kiutawala na kihisia lengo likiwa kuzifanya mahkama hizo zitekeleze majukumu yake kwa wepesi na uadilifu unaotakiwa chini ya sheria mama ya nchi ambayo ni Katiba. Mahkama haitakiwi kulazimishwa au kupokea vitisho vya aina yoyote.

Ni wazi kuwa uhuru wa Mahkama ni suala la msingi na lenye umuhimu mkubwa. Kutokana na sababu hizo Serikali katika muda wote imechukua juhudi za makusudi za kuifanya Mahkama iendelee kuwa huru na kuhakikisha kuwa mihimili mingine haiingilii katika maamuzi yake.

Akihutubia kwenye sherehe za siku ya Sheria Zanzibar, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein amewataka majaji, mahakimu, wanasheria, mawakili na wahusika wote katika kada hii ya sheria kutekeleza majukumu yao bila ya kuwa na ubinafsi, upendeleo au athari za utashi wa kisiasa katika kutekeleza majukumu yao.

Kwa upande wa wananchi, alisema kuwa kila mmoja hana budi kufanya jitihada ya kuzielewa na kuzifuata sheria mbali mbali zinazogusa maisha yake ya kila siku na kuelewa usemi maarufu usemao "kutokujuwa sheria siyo kinga au utetezi katika makosa".

Kauli mbiu ya maadhimisho ya siku ya Sheria Zanzibar mwaka huu ni "Mahkama huru, msingi wa Utawala Bora", ambayo haina khitilafu na inakwenda sambamba na maamuzi ya Serikali ya kuimarisha utawala wa sheria, misingi ya haki za binadamu na utawala bora ikiwa ni pamoja na kuwa na Mahkama huru.

Hata hivyo, utawala bora unajengeka kwa kuwepo taasisi zilizo huru, zilizowekwa kikatiba na kisheria zenye kufanya kazi zake kwa uadilifu na mashirikiano. Kwa msingi huo, Serikali imeunda na kuimarisha taasisi kadhaa kwa lengo kuendeleza utawala bora ikiwemo Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu



*Mahakimu na Wanasheria wakiwa katika maandamano wakati wa kilele cha siku ya Sheria Zanzibar zilizofanyika katika viwanja vya bustani ya Victoria Mjini Zanzibar tarehe 10 Februari ambapo mgeni rasmi alikuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein*

wa Hesabu za Serikali, Idara ya Utawala Bora, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Uhujumu Uchumi.

Serikali inamatarajio makubwa kwamba, taasisi hizo zitaendelea kutekeleza majukumu yao ipasavyo ili iweze kuongeza kasi ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo, kukuza demokrasia na kuimarisha utawala bora.

Katika kuzidi kuimarisha masuala ya Utawala Bora, tarehe 30 Januari, 2015, Baraza la Wawakilishi lilipitisha rasmi Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambao unatarajiwa kutiwa saini na Rais siku za hivi karibuni baada ya taratibu za kisheria kukamilika.

Kukamilika kwa hatua hiyo kutaiwezesha Serikali kuwa na Sheria ya Maadili ya Uongozi wa Umma itakayotumika kwa viongozi wote wa Utumishi wa Umma na Utumishi wa Kisiasa. Serikali ina matumaini makubwa kwamba viongozi wote na wananchi wataipokea vyema sheria hiyo. Kupitia sheria hiyo, viongozi wataweza kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu, jambo ambalo litaongeza ufanisi na kupunguza manung'uniko ya wananchi katika utendaji haki na upatikanaji wa huduma.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanziabar, katika kutekeleza wajibu wake wa kuhakikisha kuwa kunakuweko utoaji wa haki katika vyombo vya sheria, imeziimarisha Mahkama ili zifanye kazi kwa ufanisi.

Bajeti ya Mahkama imeongezwa kutoka TZS bilioni 1.3 mwaka 2010/ 2011 hadi TZS bilioni 5 mwaka 2013/2014. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 284.6. Kwa upande wa majaji, Serikali imefanikiwa kuongeza idadi yao kutoka wawili mwaka 2011 hadi sita (wakiwemo wanawake wawili) mwaka 2014, sawa na ongezeko la asilimia 200. Iwapo Mahkama inahisi majaji zaidi wanahitajika, Serikali haitosita kuwaongeza wengine mara tu itakapopata mapendekezo ya majina ya mahakimu/ wanasheria wenye sifa.

Kwa upande wa Mahakimu wa ngazi mbali mbali, idadi yao imeongezwa kutoka 43 mwaka 2010 hadi 69 mwaka 2014. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 60.5. Vile vile, mazingira ya utendaji kazi yameimarishwa, ikiwa ni pamoja na kuyafanyia ukarabati mkubwa majengo ya mahkama likiwemo jengo la Mahkama Kuu Vuga, Mahkama ya Chwaka, Mahkama ya Makunduchi, Mahkama ya Kadhi Mwanakwerekwe pamoja na Mahkama Kuu ya Chake Chake Pemba ambapo ukarabati unaendelea.

Serikali imefanya jitihada za makusudi za kuimarisha Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa lengo la kuongeza uwajibikaji na umahiri wa kisheria katika usimamizi wa mashtaka. Afisi hii imeongeza idadi ya Wanasheria wa Serikali kutoka 28 waliokuwepo mwaka 2010 hadi kufikia 50 mwaka 2015. Ongezeko hili ni sawa na asilima 78.5. Ongezeko hilo limeiwezesha Serikali kuendeleza mashtaka ya kiraia kwa kuwatumia Wanasheria badala ya polisi katika mahkama za Mikoa yote na Wilaya sita. Wilaya nne zilizobakia zinatarajiwa kuwa na utaritibu huo katika mwaka wa fedha 2015/2016.

Ni dhahiri kuwa, juhudi mbali mbali zilizofanywa na Serikali, ni kielelezo thabiti cha kuhakikisha kuwa mahakama zinaendelea kuwa huru, zinafuata misingi ya utawala bora na zinakwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia, kiuchumi na kijamii yanayoendelea kutokea ndani na nje ya nchi. Mafanikio hayo yanayoendelea kupatikana katika kukuza demokrasia na utawala bora nchini, ni matunda ya juhudi na mashirikiano ya pamoja baina ya mihimili yote ya Serikali na wananchi.

Lakini pamoja na mafanikio hayo yaliyopatikana, bado zipo changamoto kadhaa zinazohitaji kupatiwa ufumbuzi ili Serikali iweze kupata mafanikio zaidi katika kuendeleza utawala bora. Ni dhahiri kwamba bado kuna malalamiko mengi kutoka kwa wananchi juu ya ucheleweshwaji wa kesi, upoteaji wa nyaraka muhimu za ushahidi pamoja na baadhi ya wananchi kukataa kufika mahakamani kutoa ushahidi pale inapohitajika kufanya hivyo. Hizi ni changamoto ambazo majaji, mahakimu, wanasheria na watendaji wengine wa taasisi zinazosimamia sheria wanapaswa kuzifahamu ili hatimaye ziweze kupatiwa ufumbuzi.

Takwimu zinabainisha kwamba kesi 29,786 zilifunguliwa katika kipindi cha miaka minne; ambapo kesi 19,952 zilitolewa maamuzi, sawa na asilimia 67 ya kesi zote zilizofunguliwa. Hata hivyo, idadi ya kesi zilizobakia asilimia 33 bado ni kubwa. Mahkama haina budi kuongeza kasi ya usikilizaji wa kesi ili zisirundikane.

Aidha, suala la unyanyasaji wa kijinsia linaendelea kubaki kuwa changamoto kubwa miongoni mwa jamii ya Wazanzibari. Katika kukabiliana na changamoto hii, vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na wananchi hawana budi kuiunga mkono kampeni iliyoanzishwa tarehe 6 Disemba, 2014 ya kupinga vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto. Mpango maalum wa miaka miwili ulioandaliwa katika kampeni hii hivi sasa unatekelezwa na taasisi zote za Serikali na za kiraia kwa kushirikiana na wananchi na washirika wa maendeleo.

Ni wazi, mafanikio makubwa zaidi yanaweza kupatikana iwapo tu kila mmoja ataendelea kutimiza wajibu wake ipasavyo.

# Taasisi za Sheria zimetoa pongezi maalum kwa Dk. Shein



*Jaji Mkuu wa Zanzibar Mheshimiwa Omar Othman Makungu*

Taasisi zinazoshughulikia masuala ya Sheria na wadau wa sekta hiyo Zanzibar, zimetoa pongezi maalum kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwa juhudi anazozichukua yeye binafsi na Serikali anayoiongoza katika kuimarisha suala la utawala bora nchini.

Akizungumza katika maadhimisho ya siku ya sheria Zanzibar, zilizofanyika tarehe 10 Februari 2015 katika uwanja wa bustani ya Victoria "Victoria Garden", Jaji Mkuu wa Zanzibar Mheshimiwa Omar Othman Makungu amesema tokea kushika madaraka ya urais mwezi Oktoba 2010, Dk. Shein amekuwa akichukua hatua mbali mbali yeye binafsi na serikali anayoiongoza katika kuweka na kusimamia vyema misingi ya utawala bora, jambo ambalo halijawahi kufanywa na kiongozi yeyote miongoni mwa viongozi waliomtangulia.

"Mhe. Rais, leo hii tunatoa shukrani zetu za dhati kwa juhudi kubwa ulizozifanya kwa mambo yafuatayo; Kwanza umeteua Majaji watano (5) akiwemo Jaji Mkuu kutoka Majaji sita (6) waliopo. Hii ni idadi kubwa ya uteuzi iliyofanywa na Rais mmoja tangu Mapinduzi ya 1964. Pili, umeteua Makadhi wote pamoja na Kadhi Mkuu na Naibu Kadhi Mkuu ukiondoa Makadhi watatu (3) kati ya Makadhi kumi na tatu (13) waliopo. Tatu, katika kipindi chako tumepewa fursa ya kuajiri Mahakimu wa ngazi mbali mbali na sasa kufikia Mahakimu 62. Aidha tumeajiri watumishi wa ngazi mbali mbali wakiwemo Makarani, Wapiga Chapa na watumishi wengine. Ni dhahiri hii ni hatua kubwa sana iliyowaongezea wananchi fursa ya kupata haki", alisema Jaji Mkuu.

Alisema kwa upande wa Majaji waliopo Zanzibar wanakidhi haja, isipokuwa idadi zaidi ya Majaji wanahitajika kwa ajili ya Mahkama ya Rufaa ya Tanzania kwa kuwa idadi ya Majaji wa Rufaa kutoka Zanzibar iliyopo sasa ni ndogo mno. Rais wa Zanzibar aliahidi kuongeza idadi ya watendaji wa mahkama wakati wowote atakapowasilishiwa mahitaji ya majaji na mapendekezo ya watendaji wenye sifa.

Miongoni mwa mambo yaliyofanywa na Dk. Shein katika kuimarisha utawala bora katika kipindi chake cha uongozi ni pamoja na kuanzisha Wizara inayoshughulikia masuala ya utawala bora, kuanzishwa kwa chombo kinachosimamia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi na hivi karibuni kupitishwa kwa Mswada wa Maadili ya Viongozi ambao sasa unangojea idhini ili kuwa sheria.

Sheria ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi na Sheria ya Maadili ya viongozi ni sheria mbili muhimu katika nchi inayofuata misingi ya utawala bora, na zinapaswa kujulikana zaidi na wananchi hasa wakati huu ambapo tupo katika maandalizi ya uchaguzi mkuu. Suala la rushwa ni suala zito na linazihusu taasisi mbali



*Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Bwana Said Hassan Said*

mbali zinazotoa huduma kwa wananchi ikiwemo Mahkama, vyama vya siasa, wagombea wa nafasi za kisiasa na wengine wengi. Aidha, sheria ya Maadili ya Viongozi ni muhimu ili kuweza kuchuja viongozi wenye maadili mazuri.

Kuwepo kwa Mahkama huru ni moja ya misingi ya utawala bora kwani kukosekana kwa mahkama iliyo huru na inayotoa haki kwa wananchi inaweza kupelekea kukosekana kwa amani na utulivu katika nchi.

"Mhe. Rais, tunakushukuru wewe binafsi na Serikali kwa jitihada zinazofanywa ili Mahkama na Taasisi za kusimamia haki zifanye kazi zao kwa weledi zaidi, hasa kwenye kuongeza fursa ya kupata haki", alisema Jaji Mkuu.

Kuhusu Mahkama, Jaji Mkuu alisema katika kipindi chake cha uongozi ambacho sasa kinaingia mwaka wa tano, Dk. Shein ameweza kutatua changamoto nyingi zilizokuwa ni kikwazo si tu kwa mahkama kutenda haki bali vile vile kwa wananchi kupata fursa ya kupata haki sawa na kwa wakati. Baadhi ya vikwazo hivyo vilikuwa uhaba wa watumishi hasa Majaji, Mahakimu, Makadhi, bajeti ndogo na isiyokidhi mahitaji halisi na majengo chakavu ya Mahkama.

Kwa upande wa majengo ya Mahkama, Serikali imewezesha kufanywa ukarabati mkubwa wa jengo la Mahkama Kuu Vuga, Mahkama ya Makunduchi, Mahkama ya Kadhi wa Wilaya Mwanakwerekwe na sasa ukarabati mkubwa unaendelea katika Mahkama ya Chake Chake Pemba.



*Mkurugenzi wa Mashtaka Bwana Ibrahim Mzee Ibrahim*



*Rais wa Mawakili Zanzibar Bwana Awadh Ali Said*

# Zingatieni sheria na kanuni za utumishi wa umma – Dk. Shein



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein (kulia) akizungumza na Uongozi wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora katika mkutano uliozungumzia utekelezaji wa mpango kazi na bajeti wa Wizara ya hiyo kwa kipindi cha mwezi Julai-Disemba 2014 katika ukumbi wa Ikulu Mjini Zanzibar uliofanyika tarehe 17 Februari, 2015*

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein kwa mara nyengine tena amesisitiza umuhimu wa viongozi na watendaji wa Ofisi yake kufanyakazi kwa bidii huku wakizingatia sheria na kanuni za utumishi wa umma kama zilivyoelezwa kwenye Sheria Nambari 2 ya Utumishi wa Umma ya mwaka 2011.

Dk. Shein amerejea wito huo wakati alipokuwa akizungumza na uongozi na watendaji wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi baada ya kuwasilishwa na kujadiliwa taarifa ya utekelezaji ya Wizara hiyo kwenye mkutano wa kutathmini utekelezaji wa bajeti na mpango kazi kwa kipindi cha miezi sita kuanzia mwezi Julai – Disemba 2014.

Amesema suala la kutekeleza majukumu ya kazi kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma linamuwajibikia kila kiongozi na mtendaji wa Serikali, ambaye katika kazi zake za kila siku anapaswa kujielekeza zaidi katika malengo yake ya kazi, kujielekeza kwa watu anaowapa huduma, kushiriki pamoja na kufanya matumizi ya fedha na raslimali nyengine kulingana na thamani halisi ya matumizi husika.

Rais wa Zanzibar mara kwa mara amekuwa akitoa wito huo kuwakumbusha viongozi na watendaji wa Wizara yake pamoja na Wizara nyingine zote za Serikali majukumu yao kwa lengo la kuhakikisha kuwa azma ya kuongeza ufanisi na kutoa huduma bora zaidi kwa jamii inafanikiwa.

Katika kuhakikisha kuwa lengo hilo linafikiwa, hatua ya kwanza iliyochukuliwa na Serikali ni kupitisha Sheria ya Utumisi wa Umma Nambari 2 ya mwaka 2011 ambayo pamoja na mambo mengine imebainisha miiko ya utumishi wa umma pamoja na kanuni za maadili ya utumishi.

Kwa mujibu wa Sheria hiyo, maamuzi ya uajiri katika utumishi wa umma wa Zanzibar yatafanywa bila ya kujuana, upendeleo au utashi wa kisiasa na uteuzi na upandishwaji vyeo katika afisi za utumishi wa umma wa Zanzibar utafanywa kwa misingi ya kuwa na sifa.

Kadhalika, sheria hiyo imebainisha kuwa miongoni mwa miiko ya utumishi wa umma ni kwamba, muundo wa utumishi wa umma wa Zanzibar utazingatia kwa kadri itavyowezekana mchanganyiko wa watu wa Zanzibar, utumishi utakuwa wenye ufanisi na uwajibikaji ambao vile vile utazingatia utoaji wa huduma bora kwa jamii.

Aidha, utumishi wa umma utazingatia kuwa utiifu kwa serikali unaendelezwa, bidii ya kazi inazingatiwa, sheria zinaheshimiwa, heshima kwa wote inafuatwa kwa usahihi na nidhamu na kanuni za maadili na uadilifu zinafuatwa.

Hatua nyengine iliyochukuliwa na Serikali ni kupitishwa kwa sheria ya Rushwa na uhujumu wa uchumi ya mwaka 2012, ambayo imeipa madaraka makubwa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi kufanya kazi mbali mbali zenye lengo la kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi nchini.

Mamlaka hiyo pamoja na mambo mengine imepewa jukumu la kupokea na kuchunguza malalamiko yoyote yatakayohusiana na masuala ya rushwa kutoka kwa mtu yoyote ndani au nje ya taasisi ya Serikali. Aidha, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo hatopewa amri wala shinikizo na mtu au mamlaka nyengine yoyote kuhusiana na maamuzi yake katika kutekeleza kazi yake.

Hatua nyengine ya hivi karibuni kabisa ni ile ya kupitishwa katika Baraza la Wawakilishi Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 2014. Sheria hiyo itatumika kwa viongozi wote wa utumishi wa umma na utumishi wa kisiasa ikiwa ni pamoja na wajumbe wa Baraza la wawakilishi na viongozi wa mahkama, viongozi wote wanaofanyakazi katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au wanaofanyakazi kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndani na nje ya nchi.

Chini ya sheria hiyo, maadili ya viongozi wa umma yatalenga kwa kadri iwezekanavyo kuhakikisha kuwa wanafanyakazi kwa uaminifu, ukarimu, umakini, kutosheka na kukuza maadili kwa kiwango cha juu ili imani ya wananchi katika utendaji wa Serikali bila ya upendeleo iweze kuimarika.

Aidha, kwa kuzingatia kuwa umma unawaangalia, viongozi wa umma watakuwa na jukumu la kutekeleza majuku yao ya kiofisi na kujipangia mambo yao binafsi kwa namna ambayo itazingatia kwamba jukumu hilo halikamiliki kwa kufanyakazi kwa mujibu wa sheria pekee bali kwa kuzingatia kuwa umma unawaangalia.

Kuhusu viongozi wote wa umma; wale wa kuchaguliwa au kuteuliwa, Serikali itaanzisha taratibu za kutangaza mali wanazomiliki, au madeni wanayodaiwa mwenza wake au watoto wake wadogo bila ya kuathiri haki za wenza wa viongozi wa umma kumiliki mali wao wenyewe.

Sheria ya maadili ya viongozi wa umma inatarajiwa kuanza kutumika katika tarehe ambayo Waziri mwenye dhamana ya Maadili ya Viongozi wa Umma atatangaza katika gazeti rasmi.

Kuna usemi maarufu wa Kiswahili usemao "haki na wajibu ni watoto pacha". Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikichukua juhudi maalum kuhakikisha kuwa haki za viongozi na watendaji zinalindwa na zimewekwa wazi kwenye sheria ya utumishi wa umma. Sambamba na hatua hiyo, kwa mara ya kwanza tokea Mapinduzi ya tarehe 12 Januari 1964, Serikali ya awamu hii imeinua kwa kiasi kikubwa maslahi ya wafanyakazi – mishahara na posho.



*Baadhi ya watendaji wa Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora wakiwa kwenye mkutano wa ofisi yao unaojadili mpango kazi na bajeti kwa kipindi cha miezi sita kuanzia mwezi Julai – Disemba 2014 uliofanyika Ikulu tarehe 17 Februari 2015*

Ni dhahiri, kwa kuwa Serikali imeshatekeleza haki za wafanyakazi kwa ujumla wake, hakutakiwi kuwe na vikwazo kutekelezwa kwa ukamilifu sheria hizi. Huduma zinazotolewa na Serikali kwa umma zinatazamiwa kuimarika zaidi kutokana na ukweli kwamba, mapungufu mengi ya kiutendaji yalikuwa yanasababishwa na baadhi ya watumishi wa umma kutowajibika ipasavyo katika dhamana zao walizopewa na kwamba ilithibitika kipindi kilichopita kwamba rushwa ni kweli adui wa haki.

Katika mkutano huo Rais wa Zanzibar vile vile alizungumzia umuhimu wa kuwatumia wataalamu wa ndani katika kutekeleza masuala mbali mbali ya kitaalamu ya ndani na kufuta kabisa tabia iliyojengeka ya kuwatafuta washauri elekezi kutoka nje ya Zanzibar.

Hoja ya Mheshimiwa Rais inatokana na misingi ya ukweli kwamba Wazanzibari wengi wameshaelimika kiasi ambacho kuna wataalamu wengi waliobobea katika fani tofauti. Lakini sifa nyengine ya kipekee ambayo wanaikosa washauri elekezi kutoka nje ya Zanzibar, ni kujua mazingira, mila, silka na utamaduni wa watu wa visiwa vya Unguja na Pemba ambao ndio wahusika wakuu katika kazi zinazofanywa na wataalamu hao kutoka nje.

Dk. Shein ameelezea matumainio yake kwamba wataalamu wa ndani siyo tu wanaweza kufanya vizuri zaidi ikilinganishwa na wataalamu kutoka nje, lakini malipo yao yanaweza kuwa nafuu zaidi ikilinganishwa na wale wanaotoka nje ya nchi, jambo ambalo litapelekea fedha ambazo zingetumika kuwalipa wao zikatumika kugharamia shughuli nyengine za maendeleo. Faida nyengine itakayopatikana kwa kutumia wataalamu wa ndani ni kuwajengea uwezo katika kufanya kazi walizozisomea.

Rais wa Zanzibar ametaka utaratibu maalum uandaliwe wa kuwapatia taarifa wataalamu wa ndani kila zinapotokea kazi zinazohitaji ushauri wa kitaalamu badala ya kutoa matangazo hayo kupitia kwenye vyombo vya habari pekee, kwani alisema baadhi ya wataalamu hao ama hawana muda wa kutosha kuweza kusoma magazeti au maeneo yao ya kazi hayatoi fursa ya kupokea magazeti ya kila siku.

"tuwatumieni wataalamu wetu wa ndani iwe katika Wizara husika au ndani ya serikali yenyewe, tusitoke nje, tukumbuke methali maarufu ya marehemu kiongozi wetu – tukuza kilicho chako mpaka usahau cha mwenzako" alisema.

# Madaktari bingwa kutoka Uingereza wamekutana Zanzibar

## Dk. Shein amealikwa rasmi kutoa mhadhara



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akihutubia kwenye mkutano maalum wa wataalamu wa maradhi yanayohusiana na mfumo wa utoaji wa haja ndogo kutoka nchini Uingereza uliofanyika katika ukumbi wa Hoteli ya Breezes iliyoko Bwejuu Wilaya ya Kusini Mkoa wa Kusini Unguja tarehe 20, Januari 2015*

Mandhari ya Zanzibar inayopambwa na hali ya amani na utulivu imeendelea kuwa kivutio kikubwa isiyo tu kwa watalii ambao idadi yao imekuwa ikiongezeka siku hadi siku, lakini vile vile kwa wataalamu wa fani tofauti ambao wamekuwa wakiwasili kwa lengo la kufanya mikutano kwenye hoteli mbali mbali.

Wakati Serikali imeripoti ongezeko la asilimia 107 ya watalii wanaokuja kutembelea Zanzibar kutoka mwaka 2010 hadi mwaka 2014 kutokana na mazingira bora yanayoruhusu kuendeleza biashara hiyo, makundi ya wataalamu na watu mashuhuri nao wamekuwa wakimiminika kwa wingi Zanzibar kwa shughuli tofauti ikiwemo kupumzika, kufanya utafiti na kuendesha mafunzo ya muda mfupi.

Mwezi Januari mwaka huu, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alialikwa kwenye mkutano maalum wa wataalamu wa maradhi yanayohusiana na mfumo wa utoaji wa haja ndogo kutoka Uingereza ambao kwa mwaka huu wameichagua Zanzibar kuwa ni sehemu ya kufanyia mkutano wao. Mkutano huo ulifanyika kwenye ukumbi wa Hoteli ya Breezes iliyoko Dongwe, Mkoa wa Kusini Unguja.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wataalamu hao – "Royal Society of Medicine – Urology Section", Dk. Roger Plail, uamuzi wao wa kuja Zanzibar kufanya mkutano huo wa wataalamu umetokana na mashirikiano mazuri yaliyopo kati yao na Madaktari wa Zanzibar na vile vile hali ya amani na utulivu, mambo ambayo yaliwahakikishia kuufanya mkutano wao huo kwa ufanisi.

Akizungumza kwenye mkutano huo, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alitumia fursa hiyo kuelezea historia ya Zanzibar kisiasa, kiuchumi na kijamii pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kuimarisha sekta ya afya nchini ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa Sera katika sekta hiyo.

Katika kipindi cha miaka minne iliyopita, idadi ya madaktari na wataalamu mbali mbali wa afya Zanzibar imeongezeka kutoka 3,634 mwaka 2010 hadi kufikia 4,618 mwaka 2014. Ongezeko hili ni sawa na asilimia 26.

Sambamba na ongezeko hilo, idadi ya madaktari wazalendo walioajiriwa nayo sasa imeongezeka kutoka madaktari 62 hadi kufikia 102 baada ya kuajiriwa madaktari wazalendo 37 katika mwezi wa Novemba, 2014. Hivi sasa Zanzibar wapo madaktari 40 wa kigeni. Kwa jumla, idadi ya madaktari wote wanaotoa huduma Zanzibar, sasa imefikia 142.

Kwa idadi hiyo ya madaktari na idadi ya watu wa Zanzibar, kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, hivi sasa daktari mmoja anatoa huduma kwa watu 9,708. Kiwango hiki cha madaktari kimesaidia sana katika utoaji wa huduma za afya kwa Unguja na Pemba. Hata hivyo, jitihada za kuwasomesha madaktari na watalaamu wengine wa afya zinaendelezwa.

Kwa mfano, katika kuhakikisha kuwa idadi ya Madaktari inaongezeka kupitia Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kukiimarisha Chuo chake cha Madaktari ambacho hivi sasa kina wanafunzi 99 waliopo mwaka wa kwanza na mwaka wa pili katika fani ya udaktari katika Chuo Kikuu hicho.

Aidha, Serikali inaendelea kukiimarisha Chuo chake cha Afya kilichopo Mbweni Zanzibar ambacho kinatarajiwa kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) pamoja na kuhakikisha kuwa Hospitali ya rufaa ya Mnazi Mmoja inafikia lengo lililowekwa sambamba na ujenzi wa hospitali ya kisasa ya Mkoani Pemba unaoendelea.

Pamoja na jitihada hizo, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar na Wizara ya Elimu ya Tanzania Bara zitaendelea kutoa mikopo ya elimu ya juu kwa wanafunzi watakaofaulu masomo ya sayansi na kujiunga na masomo ya fani ya udaktari katika vyuo mbali mbali vya ndani na nje ya nchi.

Serikali inamatumaini makubwa kwamba kutokana na juhudi hizo, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuwa imefikia kiwango cha kimataifa katika kutoa huduma za afya katika kipindi cha miaka michache ijayo, ambapo miundo mbinu ya afya Unguja na Pemba itakuwa imeimarika.

Vile vile, Dk. Shein aliitumia fursa hiyo, kutoa shukurani kwa juhudi zinazochukuliwa na Jumuiya ya Misaada ya Uingereza katika kuimarisha programu za Afya hapa Zanzibar (HIPZ), na hivyo kuunga mkono juhudi za Serikali katika kutoa na kuimarisha huduma hizo katika hospitali ya Makunduchi na Kivunge.

"Natumia fursa hii kutoa shukurani kwa Dk. Ru McDonagh na madakatari wote kwa huduma wanazozitoa katika hospitali hizi....", alisema Dk. Shein.

Dr. Ru kupitia jumuiya yake ya HIPZ tayari ameshaifanyia ukarabati mkubwa hospitali ya Makunduchi sambamba na kuweka vifaa vyote muhimu vya uchunguzi wa maradhi pamoja na kukifanyia matengenezo chuma cha upasuaji ambacho kimeshaanza kutoa huduma ikiwemo huduma za dharura za upasuaji kwa kinamama wajawazito wanaoshindwa kujifungua kwa njia ya kawaida.

Dk. Shein ambaye ni mtaalamu katika fani ya Patholojia, alitoa shukurani kwa Jumuiya hiyo kwa kuamua kufanya mkutano huo hapa Zanzibar huku akieleza azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuwapata wataalamu wakiwemo wa maradhi yanayohusiana na haja ndogo na maradhi mengineyo.

Akizungumza katika kilele cha maadhimisho ya miaka 51 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alielezea mipango ya Serikali katika kuimarisha huduma za afya ambapo alisema serikali iko mbioni kuhakikisha kuwa huduma za maradhi ya figo zinapatikana hapa Zanzibar na kazi hiyo tayari imeshaanza kutekelezwa kwa ujenzi wa jengo litakalotoa huduma hizo.

Ni dhahiri, hatua hiyo inakwenda sambamba na malengo ya SMZ katika kuimarisha huduma za jamii kwa upande wa sekta ya afya.

Mkutano huo umehudhuriwa vile vile na madaktari bingwa wa maradhi hayo kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.



*Baadhi ya washiriki wa Mkutano wa madaktari kutoka nchini Uingereza wakimasikiliza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamaed Shein kwenye mkutano maalum wa wataalamu wa maradhi yanayohusiana na mfumo wa utoaji wa haja ndogo kutoka Uingereza uliofanyika katika ukumbi wa Hoteli ya Breezes iliyoko Bwejuu Mkoa wa Kusini Unguja tarehe 20 Januari 2015*

# SMZ imeendelea kutekeleza uimarishaji wa Afya ya wazazi, watoto wadogo na wachanga

## Tatizo la ajira kwa vijana nalo limeshughulikiwa ipasavyo



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa Tanzania Alvaro Rodriguez ambaye aliongoza ujumbe wa Wakuu wa Taasisi za Umoja wa Mataifa wenye Ofisi zao Nchini Tanzania ulipofika Ikulu Mjini Zanzibar tarehe 13 Februari 2015*

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea kuweka kipaumbele katika kuimarisha afya ya wazazi, watoto wadogo na watoto wachanga kwa lengo la kupunguza idadi ya vifo ili hatimaye iweze kufikia malengo ya Maendeleo ya Milenia ya Umoja wa Mataifa.

Kwa lengo la kupunguza vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga, Serikali imekuwa ikihimiza utekelezaji wa uamuzi wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi uliotolewa mwezi wa Mei, 2012 kwamba akinamama wajawazito wakajifungue kwenye vituo vya afya na hospitali za Serikali bila ya malipo yoyote pamoja kuhudhuria kwenye kliniki wakati wa kipindi cha ujauzito.

Aidha, ujenzi wa kliniki umeendelea kufanyika katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba na taarifa za Wizara ya Afya zinaeleza kuwa, hakuna eneo la Zanzibar ambalo wananchi wake wanaweza kutembea umbali wa kilomita tano bila ya kukuta kliniki, hatua ambayo haijawahi kufikiwa na mataifa yote ya bara la Afrika.

Hatua nyengine za Serikali katika kuthibitisha utekelezaji uimarishaji wa afya ya jamii, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein katika hotuba yake ya kuadhimisha miaka 51 ya Mapinduzi ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari 1964, alisisitiza umuhimu wa wafanyakazi wa vituo vya afya na wodi za wazazi za Serikali, kutowatoza malipo ya aina yoyote wazazi wanapokwenda kujifungua kwa njia ya kawaida au ya upasuaji, kwani huduma hizo zinapaswa zitolewe bure.

Sambamba na hatua hiyo, Serikali imekuwa ikitoa taaluma kwa jamii kuhusiana na umuhimu wa akinamama kujifungua hospitalini.

Dk. Shein alisema hayo katika mazungumzo kati yake na ujumbe wa wakuu wa Taasisi za Umoja wa Mataifa zenye ofisi zake nchini Tanzania ambao ulifika Ikulu kumsalimia.

Hata hivyo amesema, ingawa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepiga hatua kubwa katika kuyafikia baadhi ya Malengo ya Milenia, suala la kupunguza idadi ya vifo vya mama wajawazito na watoto wachanga limebaki kuwa changamoto kubwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama ilivyo kwenye mataifa mengine yaliyo Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Alisema changamoto kubwa katika kufikia Malengo ya Milenia kwenye eneo hilo inatokana na ukosefu wa wataalamu wa kutosha wenye sifa kwenye hospitali mbali mbali za

Unguja na Pemba na uelewa mdogo wa jamii kuhusu umuhimu wa wazazi kujifungulia kwenye vituo vya afya.

Hata hivyo, amesema Serikali imechukua juhudi kubwa katika kukabiliana na changamoto hiyo ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya madaktari na wataalamu mbali mbali wa afya kutoka 3,634 mwaka 2010 hadi kufikia 4,618 mwaka 2014 na kwamba kwa mujibu wa idadi ya madaktari iliyopo sasa daktari mmoja anatoa huduma kwa watu 9,708.

Kwa mujibu wa ripoti ya mwaka 2014 ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia watoto UNICEF, dunia kwa jumla imepata mafanikio makubwa katika kupunguza idadi ya vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano, lakini hali inaonekana kuwa bado ni mbaya katika mataifa yaliyoko Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Ripoti hiyo imeeleza kuwa idadi ya vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano imepungua kutoka 12.7 milioni mwaka 1990 hadi kufikia 6.3 milioni mwaka 2013.

"Mataifa yote isipokuwa yale yaliyoko Kusini mwa Jangwa la Sahara, yamepunguza idadi ya vifo vya watoto kwa wastani wa asilimia 52 au zaidi ya hapo". Imeeleza sehemu ya ripoti hiyo iliyopatikana kwa njia ya mtandao.

Miongoni mwa sababu za vifo hivyo vya watoto zimeelezwa kuwa ni kwa akinamama kujifungua kabla ya wakati, matatizo yanayojitokeza wakati wa kujifungua, ukosefu wa lishe bora pamoja na malaria.

Akizungumzia suala la ajira, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein alisema kama ilivyo kwenye sehemu nyengine katika bara la Afrika na duniani kote, tatizo la ajira kwa vijana, kuimarisha maisha, lishe bora na ustawi wa jamii hasa kwa watoto, wanawake na makundi yaliyo katika mazingira hatarishi, nalo limekuwa na changamoto zake Zanzibar licha ya juhudi kadhaa ambazo Serikali imekuwa ikichukua.

Taarifa za Mashirika ya Kimataifa yanayoshughulikia maendeleo ya vijana duniani zinaeleza kuwa vijana wenye umri kati ya miaka 15 na 25 wanakisiwa kufikia zaidi ya asilimia 60 ya jumla ya idadi ya watu duniani ambapo ni kiasi cha asilimia 45 ya jumla ya nguvu kazi duniani.

Tofauti na nchi nyengine zinazoendelea, idadi ya watu katika mataifa yaliyoko Afrika na hasa Kusini mwa Jangwa la Sahara yamekuwa na idadi kubwa zaidi ya vijana ambapo takwimu zinaonesha kuwa zaidi ya asilimia 75 ya watu wanaoishi kwenye eneo hilo ni vijana.

Aidha, tafiti zilizofanywa na mashirika hayo ya Kimataifa katika maeneo mbali mbali ya bara la Afrika zimeonesha kuwa katika mataifa hayo vijana wengi wana ujuzi mdogo au hawana kabisa ujuzi wa kubuni miradi ya kuendesha maisha yao na hivyo kwa kiasi kikubwa kutengwa na maisha ya uzalishaji kiuchumi na kijamii. Vijana wachache wenye elimu, nao hawako vizuri kwani taaluma yao mara nyingi siyo tu haiwawezeshi kujiajiri wenyewe, lakini haiendani na mazingira halisi ya soko la ajira na hivyo kusababisha mamilioni ya vijana kukosa ajira.

Kwa upande wa Zanzibar hali haiko mbaya sana ambapo kwa mujibu wa taarifa za mwisho rasmi za Serikali za mwaka 2010 ni asilimia 17 tu ya vijana ambao hawana ajira. Kiasi hicho ni kidogo ikilinganishwa na baadhi ya mataifa ya Ulaya ambayo yanafikia zaidi ya asilimia 30 ya vijana wasiokuwa na ajira.

Katika kukabiliana na tatizo hilo la ajira, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha mfuko maalum wa uwezeshaji wananchi kiuchumi kwa lengo la kuwasaidia vijana, ingawa ongezeko kubwa la vijana wanaomaliza vyuo vikuu limekuwa likileta changamoto kwa Serikali. Changamoto hiyo pia inachangiwa na mfumo wa elimu ambao unaendelea kuwaandaa vijana katika mazingira ya kuajiriwa badala ya kujiajiri wenyewe.

Vile vile Serikali imeanzisha vyuo vya amali Unguja na Pemba kwa wanafunzi wanaoshindwa kuendelea na masomo yao ya elimu ya juu pamoja na kituo maalum cha kisasa chenye lengo la kuwaendeleza wajasiriamali.

Rais wa Zanzibar amezishukuru taasisi zote za Umoja wa Mataifa kwa misaada yake mbali mbali inayotoa kwa Zanzibar na kuelezea matumaini yake kwamba Mashirika hayo yataendelea kufanyakazi kwa pamoja na Serikali katika utekelezaji wa malengo mapya kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Naye kiongozi wa Ujumbe huo Mratibu Mkaazi wa Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa Bwana Alvaro Rodriguez amesema changamoto zote zilizojitokeza katika utekelezaji wa malengo ya Milenia zinatarajiwa kuendelea kupatiwa ufumbuzi kwenye mpango mpya ujao ambao utajumuisha masuala ya Maendeleo ya Uchumi, Ustawi wa Jamii, na Utawala Bora, Demokrasia na Maendeleo.



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na ujumbe wa Wakuu wa Taasisi za Umoja wa Mataifa wenye Ofisi zao Nchini Tanzania ulipofika Ikulu Mjini Zanzibar tarehe 13 Februari 2015*

# Matukio katika Picha



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na Balozi wa Rwanda Nchini Tanzania Eugene S.Kayihura alipofika Ikulu Mjini Zanzibar tarehe 6 Februari 2015



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapnduzi Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein akiangalia kitabu kwenye maonesho maalum ya maadhimisho ya kutimia miaka 90 ya Skuli ya sekondari ya Benbella tarehe 8 Februari 2015. Kulia kwa Mhe. Rais ni Dk. Yussuf Nuhu Pandu Mwenyekiti wa Maonesho hayo.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alhaj Dk. Ali Mohamed Shein akikata utepe kuifungua Madrasatul Al-Tawheed iliyopo Kiongoni Makunduchi Wilaya ya Kusini Unguja tarehe 21 Februari, 2015



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akizungumza na Waziri wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Kiislamu ya Iran Mohammed Javad Zarif alipofika Ikulu Mjini Zanzibar tarehe 5 Februari 2015*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein na mgeni wake Rais wa Shirikisho la Serikali ya Ujerumani Mhe. Joachim Gauck wakiangalia Ngoma ya mwanandege ambayo huchezwa katika sherehe mbali mbali za Kitaifa*



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiwaangalia wanafunzi wa Maandalizi wa Skuli ya Mkunazini Mjini Unguja Darasa la tatu (3) ambao wanatumia kompyuta kwa njia ya kusoma Vitabu wakati alipotembelea maonesho ya maadhimisho ya kutimia miaka 90 ya Skuli ya Sekondary ya Benbella tarehe 8 Februari, 2015*

# "Tutumieni misikiti kutuunganisha ili tuwe wamoja" - Dk. Shein



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alhaj Dk. Ali Mohamed Shein akikata utepe kuufungua Msikiti Mpya wa Kijiji cha Kiongoni Makunduchi, Wilaya ya Kusini Mkoa wa Kusini Unguja tarehe 21 Februari, 2015*

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Alhaj Dk. Shein amewakumbusha waumini wote kutambua kuwa misikiti ni nyumba za Mwenyezi Mungu hivyo hazinabudi kutumika kufanya mambo mema ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha waumini wa dini na siyo kuwatenganisha au kuwagombanisha.

Alhaj Dk. Shein alisema kuwa haitokuwa vyema kusikia mizozo ikiwa ni pamoja na kugombania uongozi wa msikiti miongoni mwa viongozi au Waislamu katika misikiti kwa sababu mbali mbali kwani matokeo hayo yatakuwa ni kinyume na malengo na azma ya kuuimarisha misikiti na kutozitumia vyema neema na fadhila za Mwenyezi Mungu.

Rais wa Zanzibar alieleza matumainio yake kwamba pamoja na kuwa baadhi ya wakati wapo wanaokhafilika na kufanya hivyo, imani yake ni kuwa waumini watafuata nyayo za mashehe na Maulamaa waliopita katika kufuata matendo mema ya Mwenyezi Mungu.

Dk. Shein aliyasema hayo alipokuwa akifungua msikiti huko Kiongoni Makunduchi, Wilaya ya Kusini Mkoa wa Kusini Unguja na kuelezea dhana nzima ya ujenzi na ushughulikiaji wa misikiti.

Alisisitiza kuwa msikiti huo pamoja na madrasatul alizozifungua ziwe ni chemchem ya elimu mbali mbali ikiwa ni pamoja na usomaji Kuran, Fikhi na taaluma nyengine za dini, malezi na imani.

"Mkimuona mtu anajishughulisha shughulisha na misikiti, basi shuhudieni kwa mtu huyo, imani ya kweli", Hii ni moja ya hadithi ya Bwana Mtume Muhammad (S.A.W) inayohimiza kuhusu umuhimu wa kuishughulikia na kuitunza misikiti.

Kwa mnasaba wa hadithi hiyo, Dk. Shein alisema kuwa hatua ya kuufungua msikiti huo imefikiwa kutokana na waislamu wa waliozaliwa katika kijiji hicho kuamua kwa makusudi kuushughulikia msikiti wao na kuujenga upya.

"Sote tunashuhudia mlivyo na imani ya kweli. Tumuombe Mwenyezi Mungu atulipe fadhila njema na atudumishe katika Imani na Ucha Mungu", alisema Alhaj Dk. Shein.

Ujenzi wa msikiti na madrasa ni miongoni mwa mambo ya kheri na yenye umuhimu katika kuuendeleza Uislamu. Mwenyezi Mungu anahimiza kutumia neema alizowaruzuku wanaadamu ikiwa ni pamoja na uzima wa afya, elimu na mali katika mambo ya kheri ili yapatikane malipo mema hapa duniani na huko akhera.

Katika Qur-an tukufu, aya ya 92 ya Suratul Al Imran Mwenyezi Mungu, Subhana Wataala anakumbusha

kwa kusema "Hamtaweza kuufikia wema (khasa) mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda; na chochote mnachokitoa, basi hakika Mwenyezi Mungu anakijua".

Akitoa nasaha zake mara baada ya kuufungua msikiti huo, Alhaj Dk. Shein alisema kuwa ni dhahiri kuwa kukamilika kwa ujenzi wa msikiti huo kumetokana na michango ya Waislamu katika hatua mbali mbali ambapo wapo waliotoa wazo la ujenzi, waliochangia nguvu zao, waliotoa miongozo na waliotoa fedha, ambao wote wana kheri kubwa mbele ya Mwenyezi Mungu kwani ni ishara ya watu wema.

Alielezea matarajio yake kwamba msikiti huo pamoja na madrasatul alizozifungua zitakuwa ni chemchem ya elimu mbali mbali ikiwa ni pamoja na usomaji Kuran, Fikhi na taaluma nyengine za dini, malezi na imani.

Alhaj Dk. Shein alisema kuwa Kiongoni imetoa watu mbali mbali wenye maarifa makubwa kama marehemu Mzee Sheikh Idrisa Abdul Wakil ambaye alitoa mchango mkubwa katika maendeo ya nchi na sio wananchi wa Kiongoni na Makunduchi pekee yake bali wa Taifa zima.

Katika nasaha zake hizo Alhaj Dk. Shein, aliwasisitiza waumini kuendelea kuhimizana juu ya umuhimu wa kuendeleza amani iliyopo kwa manufaa yao na vizazi viliopo na kuwataka wazazi kutochoka kusimamia malezi bora ya watoto wao na kuwaelekeza katika maadili mema sambamba na mienendo inayozingatia utamaduni na mafundisho ya dini.

Alhaj Dk. Shein alisema kuwa ujenzi wa misikiti na madrasa ni masuala ya kheri na yenye umuhimu katika kuuendeleza Uislamu. Mapema kabla ya ufunguzi wa Msikiti huo, Alhaj Dk. Shein alifungua madrasatul Tawheed iliyopo katika kijiji hicho cha Kiongoni Makunduchi.

Wanakijiji wa Kiongoni wakisoma risala yao walieleza kuwa wazo la kujenga msikiti huo lilitolewa kiasi cha miaka 110 iliyopita kutoka kwa mababu zao na kuishukuru familia ya Bwana Ali Kitambo kwa kukubali kutoa ardhi yao kuwa ni Wakfu.

Baada ya kijiji hicho kupanuka msikiti huo uliendelea na ujenzi kwa msaada wa mfadhili Sheikh Mwinyi Mohamed Kitovu na baadae ulifanyiwa matengenezo na marehemu Sheikh Idrisa Abdulwakil pamoja na Sheikh Ibrahim Ali Suleiman na Sheikh Mustafa Ali Suleiman.

Mwaka 2013, Mwakilishi wa Jimbo hilo la Makunduchi nae aliomba kuufanyia matengenezo zaidi na ndipo wanakijiji hao wakamuomba kuuzidisha msikiti huo ili uwe mkubwa zaidi.

Hafla ya uzinduzi wa msikiti na madrasa katika kijiji cha Kiongoni siku hiyo, ilitanguliwa na hafla ya uzinduzi wa Madrasatul Muzdalifa Al-Qadiria Shafii katika kijiji cha Mzuri Makunduchi ambapo Alhaj Dk. Shein alisisitiza haja ya kuzitumia Madrasa kama zilivyokuwa zikitumiwa na wazee hapo siku za nyuma kuwa ni sehemu ya kujenga na kuimarisha mashirikiano, mapenzi na umoja miongoni mwa Waislamu sambamba na kuwa ni kituo cha kuimarisha maadili, kutoa suluhu na nasaha kwa mambo kadhaa yaliokuwa yakiisibu jamii.

Alhaj Dk. Shein katika nasaha zake pia alitumia fursa hiyo kuelezea umuhimu wa kuimarisha mashirikiano baina ya wazazi, walimu na jamaii yote kwa jumla katika kuwaepusha watoto na wanawake katika vitendo vya udhalilishaji.

Alisema kuwa jukumu la kuwalinda watoto na wanawake ni la watu wote na na kwamba vitendo vya udhalilishaji wa watoto ni kinyume na maadili na haki za binaadamu, hivyo havipaswi kufumbiwa macho kwani vinatoa taswira mbaya kwa jamii na mustakbali wa maisha ya watoto.

Alhaj Dk. Shein alisema kuwa Serikali kwa kushirikiana na Taasisi na Mashirika mbali mbali imeanzisha Kampeni ya miaka miwili ya kupambana na ukatili dhidi ya akina mama na watoto.

Kwa kuwa elimu zote zinatokana na Mwenyezi Mungu, Alhaj Dk. Shein aliwasihi wazazi na walezi kuwahimiza vijana kufuatilia masomo ya dini sambamba na yale ya skuli kwani Serikali imekuwa ikichukua jitihada za makusudi katika kuhakikisha kuwa watoto wanapata haki yao ya elimu huku Serikali ikiimarisha mazingira ya skuli zote za Zanzibar.

Mwakilishi wa Jimbo la Makunduchi ambaye pia, ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma Mhe. Haroun Ali Suleiman nae alitumia fursa hiyo kuelezea kuwa mafanikio ya ujenzi huo wa Madrasa ya ghorofa moja yametokana na mashirikiano mazuri ya mfadhili na wananachi wa eneo hilo kupitia Kamati yao iliyo chini ya Mwenyekiti wake Mzee Makame Mudu.

Akisoma risala kwa niaba ya wa madrasa hiyo, Ustadh Ali Habib Suleiman alisema kuwa Madrasa hiyo imeanzishwa mnamo mwaka 1940 ambapo baadae iliendelezwa na Mwalimu Bi. Atamani binti Ali ambaye sasa ni marehemu kwa mashirikiano na Ustadh Ramadhan Mwinyi hadi kupata mfadhili mnamo mwaka 2013 na 2014. Hadi kukamilika kwake ujenzi wa madrasa hiyo umegharimu Shilingi za Kitanzania Milioni 37.

Alhaj Dk. Shein alikubali ombi la madrasa hiyo la kuwapatia kompyuta moja pamoja na printa yake huku akiwaahidi kuwaunga mkono pale watakapokuwa tayari kuanza ujenzi wa nyumba ya mwalimu mkuu pamoja na kuanza skuli ya maandalizi ndani ya Madrasa hiyo.



*Waumini mbali mbali wa dini ya Kiislamu waliohudhuria sherehe za ufunguzi wa msikiti wa Kiongoni Makunduchi wakiitikia dua baada ya Swala ya Adhuhuri iliyoswaliwa kwenye msikiti huo mpya baada ya ufunguzi rasmi tarehe 21 Februari, 2015*



*Uwanja wa Gofu wa kisasa kwenye hoteli ya Sea Cliff Mangapwani*

# Hoteli ya Sea Cliff imeanzisha uwanja mpya wa Gofu

## ■ Uwanja huu ni kivutio kipya cha Utalii

Visiwa vya Zanzibar vimepata umaarufu mkubwa duniani kutokana na utajiri wa historia yake, ambayo imesheheni matukio mengi yaliyoanza kufanyika kwa mara ya kwanza ndani ya visiwa hivi kuliko sehemu nyingi duniani.

Historia inatufundisha kuwa utamaduni wa kuyaweka majani ya chai kwenye kifungio ulianza Zanzibar kwenye kijiji cha Dunga mwaka 1901 wakati ambao hakukuwa na nchi yoyote ndani ya Afrika ya Mashariki iliyokuwa imeanza kufanya hivyo.

Aidha, tunasoma kwenye historia Zanzibar ni miongoni mwa nchi za mwanzo duniani kutumia taa za umeme, kuwa na miundombinu ya reli, bara bara na bandari. Vile vile, Zanzibar ilikuwa nchi ya kwanza barani Afrika kuanzisha televisheni ya rangi, nyumba za ibada za dini mbali mbali na mambo mengine mengi ya maendeleo. Huduma za simu nazo zilianza Zanzibar kuliko nchi zote za Afrika ya Mashariki. Hivyo hivyo, ilikuwa kwa huduma za posta.

Ingawa siyo watu wengi wanaofahamu umaarufu wa Zanzibar katika mchezo wa Gofu, lakini kumbukumbu zinathibitisha kwamba Zanzibar ilikuwa ni miongoni mwa nchi za mwanzo kabisa barani Afrika kuwa na Kiwanja cha Mchezo wa Gofu, ambacho kilikuwa katika eneo la Maisara – mjini Unguja, lakini kwa muda mrefu jitihada za kuundeleza mchezo huo zilififia.

Dalili zimeanza kujitokeza kuwa hivi sasa Zanzibar inaelekea kuirejesha hadhi hiyo kwa namna nyengine kulingana na mazingira yaliyopo sasa, ambapo biashara ya utalii inaonekana kushika kasi. Hali hiyo imedhihirika kutokana na wamiliki wa hoteli ya kitalii ya Sea Cliff kuanzisha kiwanja cha mchezo wa gofu katika hoteli hiyo iliyoko Kiomba Mvua – Wilaya ya Kaskazini B – Unguja.

Licha ya ukweli kwamba kiwanja hicho kinamilikiwa na wamiliki wa hoteli hiyo, manufaa yatakayotokana na kiwanja hicho yatawanufaisha wamiliki wa hoteli, wananchi wa Kiomba mvua na nchi nzima kwa jumla.

Faida za kiwanja hicho cha kisasa chenye kiwango cha kimataifa cha vishimo tisa, haziishii kwa wananchi wa Kiomba Mvua kujipatia ajira pekee, lakini uzuri wa kiwanja hicho utapelekea kuitangaza Zanzibar kiutalii duniani kote na hivyo kuongeza idadi ya watalii watakaokuja Zanzibar na hatimaye kuinua pato la taifa.

Katika hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwenye sherehe za ufunguzi wa kiwanja hicho ambayo imesomwa kwa niaba yake na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora, Dk. Mwinyihaji Makame,



amesema wawekezaji wa hoteli hiyo wana imani kuwa kiwanja hicho na hoteli kwa jumla, vitaendelea kuwa na mchango muhimu katika kutoa ajira kwa wananchi wa Kiomba Mvua na kuendeleza uchumi wa Zanzibar.

"Nimefurahi kupata taarifa kwamba wamiliki wa hoteli hii hawaoni kama kiwanja hiki ni mali yao peke yao; bali wanaona kama ni mali ya Zanzibar na watu wake. Wanapata hisia hizo kwa kuzingatia kuwa uzuri wa kiwanja hiki utatumika katika kuitangaza Zanzibar kiutalii na kimichezo duniani kote. Aidha, wana imaini ya dhati kuwa kiwanja hiki na hoteli hii kwa jumla vitaendelea kuwa na mchango muhimu katika kutoa ajira kwa wananchi wa eneo hili na kuendeleza uchumi wa nchi yetu." alisema

Ufunguzi wa Kiwanja cha Gofu chenye hadhi ya Kimataifa utachangia sana katika kurejesha sifa na umaarufu wa Zanzibar iliyoupata katika mchezo huu mwanzoni mwa karne ya 20 ambapo Zanzibar ilikuwa ni miongoni mwa nchi za mwanzo kabisa barani Afrika kuwa na Kiwanja cha Mchezo wa Gofu ambacho kilikuwa katika eneo la Maisara – mjini Unguja.

Historia inaeleza kuwa uwanja huo ulijengwa mwaka 1900 ambapo ni miaka 115 iliyopita. Ukubwa na mazingira ya kiwanja hicho ulishabihiana sana na mazingira ya kiwanja cha Sea Cliff hivi sasa. Uwanja huo ulikuwa pembezoni mwa bahari, wenye vishimo 9 sawa na ule wa Sea Cliff . Idadi hiyo ni nusu ya vishimo vinavyokuwemo kwenye viwanja vinavyotumika kwa mashindano makubwa ya Kimataifa ambayo yana jumla ya vishimo 18.

Kumbukumbu zinaonesha kwamba kiwanja hicho cha zamani kilitumika kwa mashindano ya Kimataifa. Miongoni mwa makombe maarufu yaliyoshindaniwa kwa wakati huo ni Kombe la Nicole ambalo kwa mwaka 1924 mshindi wake alijulikana kwa jina la Gott. Mashindano hayo yalisita kwa miaka kadhaa baada ya mwaka huo, na maendeleo ya mchezo huu yalizidi kuzorota wakati wa vita vya pili vya dunia.

Zipo kumbukumbu zinazooonesha kuwa mashindano mengine makubwa ya gofu yalifanyika tena Zanzibar mwaka 1953. Baada ya Mapinduzi kiwanja hicho kiliendelea kutumiwa kwa muda na wananchi wa Zanzibar. Eneo ilipokuwepo klabu ya gofu ya wakati huo ni pale ulipo mkahawa wa Maisara hivi sasa.

Historia hii inadhirisha ukweli kwamba Zanzibar ilizitangulia nchi nyingi za Afrika katika maendeleo ya kiuchumi, sayansi na teknolojia, kijamii na kimichezo. Zanzibar ina kila haki na sababu ya kujivunia, kuilinda na kuidumisha historia kubwa ya nchi, ambayo inaendelea kwa namna ya pekee kuwa kivutio kikubwa cha wataalii na wawekezaji kutoka pande zote za dunia.

Ni dhahiri ufunguzi wa Kiwanja hichi unakwenda sambamba na juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Awamu ya Saba za kuimarisha Sekta ya utalii ambayo ndiyo sekta kiongozi kwa uchumi wetu. Utalii hivi sasa unachangia aslimia 80 ya fedha za kigeni na una mchango wa asilimia 27 katika Pato la Taifa.

Mafaniko makubwa yanaendelea kupatikana katika Utekelezaji wa dhana ya "Utalii kwa Wote" ambayo ina lengo la kuhakikisha kuwa kila mwananchi ananufaika na matunda ya utalii na sekta ya utalii inatumika katika kuimarisha sekta nyengine za kiuchumi ikiwemo Kilimo, ujasiriamali pamoja na kukuza soko la ajira.

Juhudi za wananchi katika kuitelekeza dhana ya utalii kwa wote zimepelekea kuongezeka idadi ya watalii wanaoitembelea Zanzibar mwaka hadi mwaka. Takwimu zinaonesha kuwa Idadi ya watali 132,836 waliitembelea Zanzibar katika mwaka 2010 ambapo katika mwaka 2014 watalii wapatao 274,619 waliwasili Zanzibar. Hilo ni ongezeko la asilimia 107.

Serikali inaendeleza jitihada mbali mbali za kuimarisha maeneo yenye kumbukumbu za mambo ya kale na urithi wa utamaduni yaliyo katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba kwa lengo la kuhakikisha kuwa Utalii wa Zanzibar unawavutia wageni wenye hamu ya kuona na kuburudika na mambo mbali mbali, wakiwemo wapenda fukwe na bahari, wapenda historia, wapenda amani, wapenda utamaduni na urithi, wanaependa kulala kwenye chumba cha hoteli kilichoko chini ya bahari, na hivi sasa, wapenzi wa mchezo huu wa gofu.

Serikali inathamini sana michango na mashirikiano kutoka kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kwa kuwa tayari kuwekeza katika mambo hayo ambayo kwa kweli ni kivutio kikubwa kwa watalii.

Kwa upande mwengine, ufunguzi wa Kiwanja hicho cha Gofu unakwenda sambamba na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya Awamu ya Saba ya kuimarisha sekta ya michezo nchini. Serikali imekuwa ikishajihisha ushiriki wa wananchi na wanafunzi maskulini katika michezo mbali mbali. Lengo ni kuona kuwa vugu vugu la michezo linarejea Zanzibar na Zanzibar inatoa wanamichezo wenye vipaji mbali mbali, wenye uwezo wa kushiriki na kushinda katika mashindano ya kimataifa.

Hivi karibuni Serikali imefufua mashindano ya riadha katika ngazi ya Taifa na juhudi zinaendelea kuchukuliwa kufufua ligi za michezo mbali mbali katika ngazi zote. Hivyo kuwepo kwa uwanja huo wa gofu kutapelekea Zanzibar kuwa na wanamichezo wenye vipaji vya kucheza mchezo huu na kushiriki na kushinda katika michuano ya Kimataifa.

Bado ni mapema kufikiria kuwa na Tiger Wood kutoka Zanzibar, lakini hakuna sababu ya kuondoa matumaini kwamba hatuwezi kuwa na nyota wa aina hiyo.

Kwa hivyo, ni vyema uongozi wa hoteli hiyo, ukalipa umuhimu suala la utoaji wa mafunzo na kuwashirikisha wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla katika mchezo huu kwa kutumia kiwanja hicho kipya.




*Mama Mwanamwema Shein akikabidhi msaada mbali mbali ya chakula kwa wananchi wa Kijiji cha Matemwe tarehe 7 Julai 2014*



*Mama Mwanamwema Shein akikabidhi msaada mbali mbali ya chakula kwa wananchi wa Kijiji cha Uzini tarehe 26 Mei 2014*

# Penye nia pana njia

## Wake wa viongozi watumia Sh. milioni 135 kuyasaidia makundi ya kijamii Zanzibar

Jumla ya shilingi milioni 135 za Tanzania zimetumika kutoka katika mfuko wa Wake wa Viongozi wa Chama cha Mapinduzi CCM ambao hutumika kwa lengo la kuyawezesha makundi mbali mbali ya kijamii Unguja na Pemba.

Mke wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mama Mwanamwema Shein, aliyasema hayo wakati alipokuwa akizungumza katika sherehe ya kuyawezesha makundi mbali mbali ya kijamii katika Jimbo la Bububu, ambapo Mbunge wa Jimbo hilo, alichangia fedha na vifaa mbali mbali vyenye thamani ya shilingi milioni 6.600.

Sherehe hiyo ilifanyika katika Viwanja vya Skuli ya Bububu Mjini Unguja, ambapo Mke wa Makamu wa Pili wa Rais, Mama Asha Suleiman Iddi, alimuakilisha Mama Mwanamwema Shein kwenye hafla hiyo.

Akisoma taarifa ya Umoja huo kwa niaba ya Mama Mwanamwema Shein, Mke wa Makamu wa Pili wa Rais Mama Asha Suleiman Iddi alisema umoja huo, tayari umeshatumia fedha hizo ikiwa ni hatua ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kuyawezesha makundi ya Vijana, Wanawake na Watoto.

Alisema sera ya CCM, inaelekeza namna ya kuwawezesha wanawake na watoto pamoja na vijana na ndio maana umoja wao uliamua kuchukua hatua ya kuwapatia vifaa mbali mbali vitavyowasaidia kubadili maisha yao, kwa kuzingatia utoaji huo ni kwa watu wote bila ya kujali itikadi ya dini, kisiasa au jinsia.

Alisema, Umoja huo ambao unajumuisha wake wa viongozi wakuu wa CCM, Wabunge, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na viongozi wa Jumuiya za Chama hicho, umeamua kutoa fedha hizo, ikiwa ni sehemu ya kuisaidia serikali kufanikisha malengo yake ya kuihudumia jamii kwa njia tofauti ili hatimaye kujikwamua kutokana na hali ngumu ya maisha na hivyo kwenda sambamba na ilani ya CCM ambayo matayarisho yake yamezingatia kikamilifu mipango mikuu ya kitaifa na kimataifa – Mkuza II, Malengo ya Millenia na Dira 2020.

Imeelezwa kwenye ilani ya CCM kwamba kwa kutambua umuhimu wa makundi mbali mbali katika jamii kama vile vijana, wanawake, watu wenye ulemavu na makundi mengine, Serikali itaweka mazingira maalum kuhakikisha kuwa sera na sheria mbali mbali zinapitiwa ili kujenga mazingira yaliyo bora zaidi yatakayosaidia kuharakisha maendeleo ya makundi hayo.



*Mama Mwanamwema Shein na Mama Asha Suleiman Iddi wakikabidhi misada ya vitu mbali mbali kwa*





*Mama Mwanamwema Shein akikabidhi vifaa vya michezo kwa vijana wa Mkoa wa Kaskazini Unguja tarehe 17 Mei 2014*

Kwa mfano kwa upande wa vijana, Serikali inatambua kwamba ukosefu wa ajira, kukosa ujuzi na maarifa ya kisasa pamoja na mitaji ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazowakabili vijana wengi mjini na vijijini na kuwafanya washindwe kujiendeleza na kutekeleza wajibu wao wa kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa uchumi wa kisasa.

Ni dhahiri kwamba Serikali imechukuwa juhudi katika kukabiliana na changanmoto hiyo kwa kusimamia ipasavyo utekelezaji wa sera ya Maendeleo ya vijana, sera ya ajira na sheria ya kazi pamoja na kuendelea kuwahamasisha vijana kuunda vikundi vya uzalishaji mali.

Kwa msingi huo huo, Wake wa Viongozi wa CCM kwa muda mrefu sasa wamekuwa wakisaidia makundi tofauti ili yaweze kujiajiri, na hatimaye kujikomboa kutokana na hali duni ya maisha.

Akizungumzia juu ya Katiba iliyopendekezwa, Mama Shein, aliwataka wananchi hao kuuona umuhimu wa kuipigia kura ya ndio katiba hiyo, na kuachana na vitisho ambavyo vimeandaliwa na baadhi ya vyama vya upinzani vinavyowakataza kuigusa seuze kuisoma katiba hiyo.

Alisema suala la kuisoma Katiba hiyo ni moja ya jambo la msingi kwao, kwani njia hiyo ndiyo pekee ambayo kwanza; itawawezesha kuifahamu kabla ya kuipigia kura na pili; ni fursa nzuri kwao kufahamu haki zao ndani ya katiba hiyo ili itakapopita wawe na mwamko thabiti wa kuweza kudai haki zao kama zilivyolezwa kwenye katiba hiyo inayopendekezwa.

Alisema uamuzi wa Serikali wa kuzigawa nakala nyingi za katiba katika maeneo mbali mbali nchini Tanzania ni fursa nzuri itakayowawezesha wananchi kuisoma vyema katiba hiyo na kuifahamu na hivyo kuondoa ile tabia iliyokuwa imejengeka siku za nyuma ambapo sehemu kubwa ya jamii, ilikuwa haina tabia ya kuisoma wala kuifahamu Katiba ya nchi.

"kuja kwa mchakato wa katiba inayopendekezwa ni hatua muafaka kwa wananchi kuisoma katiba hiyo, kufahamu haki zao na kufanya maamuzi sahihi wakati wa kuipigia kura" alisema.

Mama, Shein, aliwataka wananchi hao kutotilia maanani kauli zinazotolewa na baadhi ya vyama vya siasa nchini kuishawishi jamii kutoshiriki kwenye kura ya maoni kwani amesema hatua hiyo itawanyima haki yao ya msingi ya kidemokrasia.

Mama Shein, aliwataka Wananchi hao, kuendeleza umoja na mshikamano uliopo nchini na kuifanya Zanzibar kuendelea kubaki katika hali ya amani na utulivu wakati wa kura ya maoni pamoja na uchaguzi Mkuu.

Naye Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, Bibi Zainab Mohammed Omar, akitoa hotuba yake kwenye sherehe hizo, alisema Wizara ya Uwezeshaji, itaendelea kutoa misaada ya aina mbali mbali ikiwemo mikopo na mafunzo kwa makundi tofauti ya kijamii na ametumia fursa hiyo kuendelea kuwashauri wananchi wa makundi tofauti kujiunga katika vikundi, ili iwe rahisi kwao kupatiwa misaada hiyo ambayo iwapo watafuata maelekezo ya wataalamu itawasaidia kubadili maisha yao.





*wananchi wa Wilaya ya Magharibi tarehe 1 Aprili 2014*




*Akinamama na akinababa wakishiriki kwenye maandamano ya kupinga vitendo vyote vinavyowadhalilisha wanawake na watoto nchini yaliyofanyika hoteli ya Bwawani tarehe 6 Februari, 2015*

# Jamii ishirikiane na UWAWAZA kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto

Katika kufikia malengo yaliyowekwa kitaifa na kimataifa ya kupambana na vitendo vyote vya udhalilishwaji wa wanawake na watoto, jamii hainabudi kushirikiana na UWAWAZA na kinamama wote katika kukabiliana na hatimaye kuvitokomeza kabisa vitendo hivyo ambavyo vimeonekana kuwa tishio kubwa kwa jamii katika siku za hivi karibuni.

Kutokana na dunia kufahamu na kuthamini umuhimu wa wanawake, kila ifikapo tarehe 8 Machi ya kila mwaka, akinamama wa Zanzibar, Tanzania na duniani kote, huungana pamoja kuadhimisha siku ya wanawake Duniani. Siku hii ya Kimataifa ilianza kuadhimishwa tokea mwanzoni mwa karne ya 20 katika nchi za Ulaya na Marekani.

Maadhimisho ya siku hiyo kimataifa, yamefuatia makubaliano kwamba masuala ya haki, maendeleo na usawa wa jinsia yanahitaji mtazamo maalum kimataifa kwenye mkutano wa Umoja wa Mataifa katika mwaka 1977, ambao ulirasimisha siku ya tarehe 8 Machi ya kila mwaka kuwa siku ya wanawake Duniani. Hapa Tanzania maadhimisho ya siku hii yalianza rasmi mwaka 1997.

Madhumuni ya msingi ya kuwa na siku ya maadhimisho ya wanawake katika mataifa mbali mbali duniani ni kufanya tathmini ya mchango wa wanawake katika jamii, kubaini na hatimae kuzifanyia kazi changamoto mbali mbali za maendeleo zinazowakabili wanawake.

Ni dhahiri kuwa hatuwezi kupuuza umuhimu huo kwa kuzingatia idadi kubwa ya wanawake waliopo katika jamii yetu ambao ni asilimia 51 ya Watanzania. Hapa Zanzibar kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya watu na Makaazi ya mwaka 2012, wanawake ni 672,892 kati ya Wazanzibari 1,303,569 sawa na asilimia 51.61.

Aidha, tafiti mbali mbali zimeonesha




kuwa wanawake wanachangia sehemu kubwa katika kutoa nguvu kazi katika shughuli za uzalishaji kwenye kilimo na pia hubeba jukumu muhimu la malezi katika familia zetu. Kwa mnasaba, huo akina mama wanayo nafasi ya kipekee ya kuleta ustawi wa jamii nchini na inawezekana kuwa hii ndiyo sababu ya kuwepo usemi mashuhuri wa kiswahili usemao "ukimuelimisha mwanamke mmoja ni sawa na kuelimisha jamii nzima."

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika awamu zake zote imekuwa ikiweka mazingatio maalum katika kuwashirikisha akinamama katika masuala mbali mbali ya maendeleo, uongozi sambamba na kuzifanyia kazi changamoto za maendeleo zinazowakabili. Tokea Mapinduzi Matukufu ya tarehe 12 Januari, SMZ imekuwa ikiweka Wizara maalum inayoyashughulikia masuala ya akinamama kwa undani zaidi.

Katika, Awamu ya Saba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein, masuala ya wanawake yanaratibiwa na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto chini ya Uongozi imara wa Mhe. Zainab Omar Mohamed na Katibu Mkuu wake ni Bi Asha Ali Abdalla ambao wote ni akinamama.

Uamuzi wa kuunganisha Wizara hiyo na masuala ya watoto inakwenda sambamba na masuala muhimu yaliyopewa kipaumbele maalum duniani. Uimarishaji wa afya ya mama wajawazito, watoto wachanga na watoto wenye umri chini ya miaka mitano, ni masuala ambayo yamekuwa yakijadiliwa kwa mapana kwenye vikao tofauti na kuwekewa sera maalum.

Changamoto kubwa zilizoibuka kwenye eneo hili hasa katika miaka ya hivi karibuni, ni kiasi kikubwa cha matukio ya udhalilishwaji wa akinamama na watoto kwenye maeneo mbali mbali. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali kwa upande wake imekuwa ikichukua juhudi maalum kuhakikisha kuwa wanawake na watoto wanaishi katika maisha bora zaidi kiafya na kiuchumi.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa bajeti na mpango kazi wa Wizara yake kwenye mkutano maalum wa kutathmini utekelezaji huo, Waziri wa Wizara hiyo Bibi Zainab Omar Mohamed amesema Wizara yake katika kipindi cha mwezi Julai – Disemba 2014 imefanikiwa vyema kutekeleza majukumu yake katika kuyahudumia makundi mbali mbali likiwemo kundi la wanawake.

Amesema katika kipindi hicho mkazo umeelekezwa katika maeneo tofauti ikiwemo kuimarisha hali za akinamama kiuchumi na kijamii, kuhakikisha kuwa mapungufu ya sheria na sera katika masuala ya uwezeshaji yanayohusu wanawake yanafanyiwa kazi pamoja na kuimarisha ubora wa huduma na upatikanaji wa hifadhi ya jamii kwa wanawake na makundi mengine yanayoishi katika mazingira magumu.

Majukumu mengine muhimu ya Wizara hii ambayo yametekelezwa kwa mafanikio makubwa ni kuwawezesha Wanawake kiuchumi kwa kuwahamasisha kuanzisha vikundi vya ushirika na SACCOS pamoja na kujishughulisha na shughuli za ujasiriamali.

Chini ya mpango huo, vikundi vya akina mama hupewa huduma za mafunzo na mara kadhaa wake wa viongozi chini ya uongozi wa Mama Mwanamwema Shein huvipitia vikundi vya kinamama na kuvipatia vifaa ili kuunga mkono jitihada zao.

Kwa upande mwengine, Zanzibar nayo imepiga hatua kubwa katika suala la kuwashirikisha wanawake katika uongozi na utoaji wa maamuzi katika Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Kwa mfano idadi ya wajumbe wanawake katika chombo hicho muhimu kinachowawakilisha wananchi na chenye jukumu la kutunga sheria ni asilimia 32.9 ya wajumbe wote.

Kwa lengo la kuwajengea uwezo zaidi wanawake, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka mikakati maalum wa kuimarisha huduma ya elimu kwa watoto wa kike kwa kuimarisha huduma ya elimu kwa watoto wa kike sambamba na kuanzisha skuli ya Sekondari za wanawake.

Jitihada nyengine zinazothibitisha dhamira ya Serikali katika kuwasaidia akinamama kukabiliana na changamoto zinazowakabili ni kuwaondolea malipo waliyokuwa wakitozwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja walipokuwa wanakwenda kujifungua, jambo ambalo lilikuwa likisababisha usumbufu mkubwa kwao.

Kadhalika, katika kukabiliana na kukomesha vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto, Serikali katika mwezi Disemba 2014, imezindua kampeni ya kupiga vita vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto kwa kushirikiana na taasisi za ndani na nje ya nchi.

Jitihada zote hizo zina lengo la kukabiliana na changamoto zinazowakabili wanawake katika jamii na maendeleo ya Zanzibar. Ni dhahiri kuwa mafanikio hayajawa ya kuridhisha ingawa tuna haki ya kujipongeza kwa tulipofikia wakati huu tunapoadhimisha siku ya wanawake Duniani.

Tutumie wakati huu kutathmini mafanikio na changamoto mbali mbali zilizojitokeza katika utekelezaji wa mipango ya Kitaifa na Kimataifa katika kuwawezesha wanawake na kuleta usawa wa kijinsia. Hiki ni kipindi cha kutathmini utekelezaji wa Azimio la Ulingo wa Beijing (1995-2015) Malengo ya Milenia na Agenda ya Umoja wa Afrika ilitamka kuwa mwaka 2015 ni mwaka wa kuwawezesha wanawake.

# Dk. Shein asisitiza umuhimu wa kuendelea kuitunza historia ya Zanzibar



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapnduzi Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein akikata utepe kufungua maonesho ya maadhimisho ya kutimia miaka 90 tokea kuanzishwa Skuli ya sekondari ya Benbella tarehe 8, Februari 2015*

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwa mara nyengine tena amesisitiza umuhimu wa kuendelea kuhifadhi matukio ya kihistoria ya Zanzibar kwa faida ya vizazi vya sasa na vitakavyokuja baadae.

Katika kufanikisha vyema utekelezaji wa suala hilo, Dk. Shein ameiagiza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuandika historia ya skuli mbali mbali Unguja na Pemba, jambo ambalo kwa kiasi kikubwa litaweza kupunguza usumbufu uliopo sasa wa kupata kumbukumbu sahihi kuhusu Zanzibar wakati wasomi na watafiti wanapotaka kutumia taarifa hizo. Kumbukumbu za historia huzisaidia taasisi husika kujielewa inakotoka, ilipo na kuiwezesha kutoa mwelekeo wa kupanga mipango mizuri ya inakokusudia kwenda.

Dk. Shein alisema hayo wakati alipokuwa akizungumza kwenye sherehe za maadhimisho ya miaka 90 tokea kuanzishwa kwa skuli ya Benbella zilizofanyika kwenye skuli hiyo iliyopo Mnazi Mmoja mjini Unguja.

"Nimefurahi kuona kuwa uongozi wa Skuli ya Benbella umeonesha mfano kwa vitendo juu ya umuhimu wa kuweka kumbukumbu na kuithamini historia ya taasisi zetu na nchi yetu kwa jumla" alisema.

Vile vile alisema amefarajika kuona kwamba uongozi wa skuli hiyo umetunza historia ya skuli ya Benbella tokea siku iliyoanzishwa, pamoja kuweka vyema kumbukumbu



*Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein akiangalia aina tofauti ya mapishi wakati alipotembelea maonesho maalum ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 90 tokea kuanzishwa kwa Skuli ya Sekondari ya Benbella tarehe 8 Februari, 2015*

zinazoonesha aina na mifumo ya uendeshaji wa masomo na mafunzo, mabadiliko ya jina la skuli, orodha ya walimu wakuu pamoja na wanafunzi waliosoma katika skuli hiyo.

Wakati wa Maadhimisho ya Sherehe za Miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar Dk. Shein aliziangiza Wizara na taasisi nyenigine za Serikali kuandika historia zao na ameelezea furaha yake kwa kuona kwamba agizo hilo linatekelezwa vyema.

Akielezea mfano wa usumbufu wanaoupata waaandishi na watafiti wakati wanapotaka kuandika historia ya Zanzibar, amesema siyo rahisi kwa sasa kupata picha ya iliyokuwa Skuli ya Gulioni, ambayo yeye (Mheshimiwa Rais) na wenzake wengi wa hapa Zanzibar waliisoma kabla ya Mapinduzi ya tarehe 12 Januari, 1964.

Ni ukweli uliowazi kwamba Skuli za zamani Zanzibar zinakumbusha mambo mengi ikiwemo michezo, masomo, wanafunzi waliosoma pamoja, walimu na watu wote ambao walijenga udugu na uswahiba wa namna mbali mbali katika maisha yao ya utoto na ujana maskulini. Maadhimisho ya sherehe hizo yaliwajumuisha baadhi ya wananchi waliobahatika kusoma Skuli hiyo ambao miongoni mwao ni viongozi katika ngazi tofauti serikalini na katika sekta binafsi.

"Nafahamu hisia zenu na nakupongezeni kwa kuja kwa wingi. Hata hivyo, bado wapo watu ambao walisoma katika skuli hii na wapo hapa hapa Zanzibar, lakini kwa namna moja au nyengine hamkubahatika kuwapa fursa ya kuhudhuria leo hii. Nina imani kwamba nao bado wana imani na mapenzi makubwa na skuli yao hii na wangelipenda kutoa mchango wao katika kuiendeleza. Waswahili wanasema "Kawia ufike". Kwa hivyo, nakushaurini muwatafute na kuwashirikisha ili nao weweze kutoa mchango wao wa hali na mali katika kuiendeleza skuli hii maarufu." Alisema Dk. Shein.

Kama zilivyo sekta nyengine, Sekta ya elimu ina historia kubwa Zanzibar ambayo ni vyema kila mtu kuisoma na kuifahamu, kwani kwa kufanya hivyo ndivyo itakuwa rahisi kuona wazi wazi na kuthamini mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya sekta hiyo katika kipindi hiki cha miaka ya 51 baada ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ya tarehe 12 Januari 1964.

Historia inatufundisha kuwa, skuli Zanzibar zilianza kufunguliwa mnamo mwaka 1890, na skuli ya mwanzo ilijulikana kwa jina la Sir Euan Smith Madressa, ambayo hivi sasa inaitwa Haile Sellasie. Skuli hii kabla ya Mapinduzi ilikuwa ikiendeshwa kwa misingi ya Kikabila. Katika mwaka 1907 wakati wa Utawala wa Ali Bin Homoud ilijengwa skuli nyengine ambayo ilikuwa kwa watoto, wajukuu na watoto wa kifalme.

Katika mwaka 1920 wakoloni waliamua rasmi kwamba elimu itakayotolewa Zanzibar iwe kwa matabaka na kila tabaka lilipewa elimu ya aina yake. Skuli hii ya Benbella ilianzishwa mwaka 1924 na ilijulikana kama ni Commercial School. Jina hili la Benbella ni jina iliyopewa Skuli hii baada ya skuli nyingi zilizokuwepo wakati wa ukoloni kubadilishwa majina baada ya kuwa mikononi mwa Serikali.

Jina la Seyyidah Matuka Secondary School lilikuwepo kabla

ya Jina la Benbella na lilitokana na Seyyida Matuka bint Humud Albusaid ambaye alikuwa ni Mke wa Mfalme wa tisa aliyetawala Zanzibar, ambaye ni Seyyid Khalifa Bin Haroub (1911 – 1960). Majina mengine yaliyowahi kutumiwa kwa skuli hii katika nyakati mbali mbali baada ya kuanzishwa kwake na kabla ya Mapinduzi ni Government Boys Primary Shool na Government Girls Secondary School.

Skuli nyengine zilizokuwepo wakati wa Mapinduzi na kupewa majina mapya kwenye mabano ni Agakhan Shool (Kidutani), Bohora Shool (Hamamni), Hindoo Union (Shangani), Bohora Continuation School (Sokomuhogo), Seyyid Khalifa (Gamal Abdil Nasser) na St. Monica (Mkunazini).

Nyengine ni St. Paul (Tumekuja), St. Joseph (Kiungani), Comorian School (Kajificheni), Seyyid Abdalla (Fidel Castro), Sir Euan Smith Madressa (Haile Sellassie), King George (Lumumba), Holmwood (Kidongo Chekundu), Teachers' Training College (Nkurumah) na Arabic Speaking School (Vikokotoni).

Katika mwaka 1935 ilifunguliwa skuli moja katika eneo la Dole ambayo ndiyo pekee iliyotoa fursa kwa watoto wa wakulima na Wafanyakazi. Skuli hiyo iliitwa 'Rural Middle School Dole'.

Tokea mwaka 1890 hadi 1963 watoto wa kinyonge waliopata elimu ya juu kwa muda huo wa miaka 73 walikuwa ni 36 tu. Hadi mwaka 1963 kulikuwa na skuli 62 za msingi zilizokuwa na wanafuzi 19,106 na skuli nne za sekondari zilizokuwa na wanafunzi 734. Watoto wengi wa wanyonge hawakuweza kujiunga na skuli hizo kwa sababu za ukabila na hali duni ya maisha ya wazee wao na hivyo hawakuwa na namna ya kupata fedha zilizokuwa zikihitajika kwa kulipia ada.

Mara baada ya Mapinduzi Matukufu ya Januari 12, 1964, Marehemu Mzee Abeid Amani Karume alitangaza rasmi, siku ya tarehe 01 Julai, 1964 kwamba skuli zote zilizokuwa zikiendeshwa kwa misingi ya kibaguzi ni mali ya Serikali na mtu yoyote anaweza kusoma katika skuli hizo. Lengo ilikuwa ni kuondoa ubaguzi na badala yake kujenga jamii yenye misingi ya haki na fursa sawa katika nyanja zote za kiuchumi na kijamii.

Watoto wa wanyonge waliweza kufaidika na fursa za elimu hasa baada ya Marehemu Mzee Karume kutangaza elimu bure, tarehe 23 Septemba, 1964.




*Wanafunzi wa Skuli ya Sekondari ya Benbella waliohudhuria maadhimisho ya miaka 90 tokea kuanzishwa kwa Skuli ya Sekondari ya Benbella tarehe 8 Februari, 2015.*

# Hali ya upatikanaji wa chakula Zanzibar ni nzuri




*Hali halisi ya upatikanaji wa vyakula vya aina mbali mbali katika Soko kuu la Mwanakwerekwe Zanzibar*

Kama kuna jambo muhimu kuliko yote katika maisha ya mwanadamu na hata wanyama, basi ni kuwa na chakula cha kutosha ambacho ndicho kinachowawezesha kuishi kwa raha na bila ya mashaka.

Tumejifunza katika historia kwamba upatikanaji wa chakula cha kutosha au cha ziada katika enzi za mababu, ndiyo ulikuwa mwanzo wa binadamu kuanza kupata muda wa kukaa na kufikiri jambo lililopelekea uvumbuzi wa mambo mbali mbali mapya katika maisha ya mwanadamu.

Kimsingi, mahitaji ya chakula yanamlazimikia kila mtu bila ya kujali umri wake, rika lake, jinsia yake au itikadi yake.

Sekta ya Kilimo hapa Zanzibar ndiyo yenye jukumu la kuhakikisha kuwa kunakuwa na chakula cha kutosha nchini kwa kutumia mbinu mbali mbali ikiwemo kilimo cha kisasa chenye kuleta tija kubwa zaidi kwa wakulima.

Ili kuhakikisha kuwa lengo la kupatikana chakula cha kutosha linafikiwa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa ikiendelea kusimamia utekelezaji wa sera na programu mbali mbali za kilimo kwa lengo la kuziimarisha.

Juhudi nyengine ni kuanzisha mradi maalum wa kuwawezesha wananchi katika sekta binafsi juu ya kilimo cha kisasa na cha kibiashara cha mazao ya viungo, mboga mboga na matunda sambamba na kuendeleza uzalishaji wa mazao ya biashara hasa karafuu, matunda na viungo na kutilia mkazo kilimo hai na kilimo mseto kwa lengo la kuhifadhi mazingira na kupunguza matumizi ya kemikali zenye sumu.

Mafanikio makubwa yameripotiwa katika kilimo cha kisasa cha mboga mboga na mazao mengine ya chakula kama vile muhogo, ndizi, viazi vitamu na mengineyo, na hivyo kupelekea kupungua uagiziaji wa aina hiyo ya chakula. Taarifa za Wizara ya Kilimo na Maliasili zinaeleza kuwa wakati Zanzibar inajitosheleza kwa mazao ya muhogo na viazi vitamu, tayari imeshapunguza uagiziaji wa mazao ya mboga mboga kutoka asilimia 80 mwaka 2009 hadi asilimi 30 hivi sasa.

Kwa lengo la kuwasaidia wakulima hasa wa mpunga, Serikali imeendeleza programu iliyoanzishwa mwaka 2011 ya kuwapa ruzuku wakulima ya asilimia 75 ya gharama za bei ya mbolea, mbegu, dawa ya kuulia magugu na huduma za matrekta. Aidha, katika kipindi hiki, zana, vifaa na nyenzo mbali




*Hali halisi ya upatikanaji wa aina mbali mbali za vyakula katika*

mbali zimenunuliwa ambapo jumla ya wakulima 61,500 wa kilimo cha kutegemea mvua walifaidika.

Vile vile mavuno ya zao la mpunga kwa jumla yaliongezeka kutoka tani 21,014 mwaka 2010 hadi tani 33,655 mwaka 2013. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 60. Juhudi za Serikali za kutoa ruzuku zimesaidia sana katika kupatikana kwa mafanikio hayo.

Mafanikio hayo yameonekana vile vile katika kujitosheleza kwa chakula miongoni mwa vyakula muhimu vinavyotumika sana Zanzibar ambavyo ni mchele, sukari na unga wa ngano. Kwa kiasi kikubwa bidhaa hizi zinaagizwa kutoka nje ya Zanzibar.

Kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji ya miezi sita Julai – Disemba 2014 ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko iliyowasilishwa katika mkutano maalum wa kujadili utekelezaji wa Mpango Kazi na Bajeti, katika kipindi cha Julai-Disemba 2014 wastani wa tani 107-147 za chakula muhimu mchele, sukari na unga wa ngano vilikuwepo nchini kwa ajili ya matumizi ya soko la ndani. Hivi sasa Zanzibar inakadiriwa kutumia wastani wa tani 11,431 za chakula muhimu kwa mwezi.

Hivyo kwa kutumia takwimu za uingizaji wa bidhaa hizo katika kipindi cha Julai- Disemba 2014, Zanzibar iliendelea kuwa na chakula cha kutosha cha aina hizo tatu katika kipindi hicho.

Hali hiyo imeleta faraja kubwa miongoni mwa wananchi wa Zanzibar na hivyo kuwafanya waweze kuendeleza majukumu yao katika hali ya utulivu na umakini mkubwa zaidi huku wakitafakari na kubuni njia bora zaidi za kujikwamua na ukali wa maisha.

Kadhalika, mwenendo wa bei za vyakula katika soko la dunia haukuonesha mabadiliko makubwa katika kipindi hicho. Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Biashara, Viwanda na masoko bei ya mchele kwa mwezi wa Julai- Septemba ilikuwa kati ya USD 428- 437 Kwa Oktoba-Disemba ilikuwa 433-450, sukari ilikuwa USD 500-680 kwa mwezi wa Julai – Septemba na USD 500-680 kwa mwezi Oktoba-Disemba. Kwa bidhaa za unga wa ngano mwezi Julai- Septemba ilikuwa kati ya USD 243-280 kwa mwezi na Oktoba- Disemba ilikuwa 245-290.

Vile vile mwenendo wa bei katika soko la ndani uliendelea kuwa wa utulivu bila ya mabadiliko kwa kipindi cha miezi sita iliyopita kutokana na serikali kuendelea kuchukua hatua maalum za kisera za kudhibiti bei zake kwa kushirikiana na wafanyabiashara.



*Soko kuu la Mwanakwerekwe na maghala ya chakula ya Zanzibar*

Ni dhahiri mafanikio hayo yanatokana na juhudi za Serikali katika kuendeleza Mapinduzi ya Kilimo. Akizungumza kwenye kilele cha maadhimisho ya miaka 51 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti waaza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein amesema Serikali inafanya jitihada mbali mbali katika kuendeleza Mapinduzi ya Kilimo ili kuongeza uzalishaji, kuwa na uhakika wa chakula na lishe.

Alisema kwa lengo la kuwasaidia wakulima hasa wa mpunga, Serikali imeendeleza programu iliyoanzishwa mwaka 2011 ya kuwapa ruzuku wakulima ya asilimia 75 ya gharama za bei ya mbolea, mbegu, dawa ya kuulia magugu na huduma za matrekta.

Aidha, katika kipindi hicho, zana, vifaa na nyenzo mbali mbali zilinunuliwa. Jumla ya wakulima 61,500 wa kilimo cha kutegemea mvua na kilimo cha umwagiliaji maji walifaidika.

Vile vile, mavuno ya zao la mpunga kwa jumla, yaliongezeka kutoka tani 21,014 mwaka 2010 hadi tani 33,655 mwaka 2013. Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 60. Juhudi za Serikali za kutoa ruzuku zimesaidia sana kupatikana mafanikio hayo.

Kadhalika, jitihada za kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji maji wa hekta 2,200 katika mabonde ya Cheju, Kibokwa na Kilombero kwa Unguja na Mlemele na Makwararani kwa Pemba zimeendelea.

Pamoja na mafanikio hayo, changamoto imeonekana kwenye sekta ya viwanda hasa katika usafirishaji wa bidhaa. Taarifa za Wizara ya biashara na masoko zinaonesha kuwa mchango wa sekta hiyo bado ni mdogo katika pato la Taifa.

Hata hivyo, mabadiliko makubwa kwenye sekta hiyo yanatarajiwa kuonekana hivi karibuni kutokana na juhudi mbali mbali zinazoendelea kuchukuliwa na serikali za kuanzishwa viwanda hapa Zanzibar vikiwemo kiwanda cha usaifu wa bidhaa za maziwa, viwanda vya usarifu wa mazao, sabuni, samani, pamoja na kuanza uzalishaji wa sukari katika kiwanda cha sukari cha Mahonda .

Serikali inaendelea na mazungumzo na muwekezaji wa kiwanda cha Coca Cola ambaye kiwanda chake kimesimamisha uzalishaji. Mapitio ya awali ya mkataba wa ukodishaji wa kiwanda hicho yamebaini kuwa serikali iliendelea kumiliki majengo ya kiwanda na kuyakondisha kwa miaka 20 hadi Septemba 2014 na kwamba serikali iliuza mitambo ya kiwanda kwa muwekezaji.

